# Nipashe

Alhamisi Agosti 29, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581783

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 22

**CANCELO ATIMKIA SAUDI ARABIA**

KUKITHIRI UKATILI

**Serikali** kuja na marekebisho Sheria ya Ulinzi, Usalama Mtoto

UKURASA 3



SAKATA LA WODI

**Spika** ampa mbunge hadi kesho awe na ushahidi rasmi

UKURASA 4



**Polisi** yapiga 'stop' kigogo CCM kuzuru Ngorongoro

UKURASA 4

WATU KUTOWEKA

# Miili mingine 10 yabainika

• **Tisa** walifukiwa wakiwa wamekaa, wamo watoto wa mganga wa kienyeji... *Endelea ukurasa 2*



## Samia achambua kasoro za SU, azipa njia mpya ya kupita

UKURASA 2



Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la Katiba, Bob Wangwe (wa pili kulia), akiteta jambo na Wakili wake, Alphonce Lusako katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana, kabla ya kusikilizwa kwa kesi waliyoifungua ya kupinga TAMISEMI kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Mvutano mkali kesi Uchaguzi wa Mitaa

UK. 19



Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhanga Mpina (kushoto) na Wakili wake, Boniphace Mwabukusi, wakitoka katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana, baada ya mashauri matatu likiwamo la kutaka kujua uhalali wa kodi iliyosamehewa ya uingizwaji sukari nchini waliyoifungua, kutajwa kwa mara ya kwanza mahakamani hapo. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

**MICHEZO** **GAMONDI ATAMBA KUANZA LIGI KIBABE** UK.24 **MAONI,** UK.6

## Samia achambua kasoro mashirika ya umma, ayapa njia mpya ya kupita

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewataka wakuu wa mashirika na taasisi za umma kuacha kujifungia na badala yake washirikishe sekta binafsi ili kupata ujuzi wa kuziendeleza ili kuleta tija.

Pia ameagiza taasisi za umma zilizoshindwa kusimamia na kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kupitia sekta na mashirika binafsi kuendeleza miradi hiyo.

"Kama mmeshindwa kuendesha au kusimamia miradi wapeni sekta binafsi waitumie au muwauzie waturudishie fedha zetu. Ssi tutumie ya nini wakati hatuna uwezo. wapewe sisi turudishe pesa yetu tufanyie mambo mengine," alisema Rais Samia jana jijini Arusha wakati akifungua kongamano la pili la wenyeviti wa bodi na wakuu wa taasisi za umma.

"Mfano wangu mkubwa ni kama Ubungo Plaza. ilipofunguliwa kila mtu alizungumza yake lakini sasa hivi hakuna. Mtu anayetaka kupatumia na Benjamini Mkapa Tower, hivyo Msajili wa Hazina hebu wapeleke hawa viongozi kwenye lile jumba wakaingie waone mradi ulivyokuwa mkubwa ila hauna faida. "Wekezeni mkiwa na uhakika kuwa fedha zitarudi. Mfano watu wa mashirika binafsi wakiwekeza hata shilingi moja watahakikisha fedha zinarudi na wanapata faida kwa kuwa wameshafanya utafiti na hapo ni baada ya kulipa kodi zote za serikali.

"Sisi tunaingiza fedha kwenye miradi hatuangalii tutarudisha na wakati mwingine ni uamuzi wa kisiasa. Natoa mifano, simlaumu mtu ila ni kuonesha fedha za wananchi zinapokwenda kutumbukizwa na hazirudi," alisema.

Rais pia alimwagiza Ofisi ya Msajili wa Hazina kuyaunganisha au kufuta mashirika na taasisi zisizokuwa na faida badala ya kulinda nafasi za watu wakiwamo viongozi katika taasisi hizo.

"Kufutwa na kuchanganywa kwa mashirika haya kuna jenga hofu na wakati mwingine. Ni hofu zisizokuwa za ulazima. Mfano na baada ya kuunganishwa na kuundwa kwa TPHPA imeleta faida. Pia imeiwezesha Tanzania kupata cheti viwango vya ubora wa kimataifa. Sasa wamejikita kwenye malengo yao na sasa wanakusanya fedha na kutoa gawio serikalini," alisema.

"Shirika tulililoliunda wenyewe kama halifanyi vizuri basi liondoke tu kwa kuwa hatuwezi kwenda kulinda nafasi za watu ilihali mashirika hayazalishi na hayana tija," alisisitiza. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof.Kitila Mkumbo, alisema katika kipindi chake cha uongozi, Rais Samia amepambana kuifungua nchi ndani na nje ya nchi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mitaji na Uwekezaji (PIC), Augustine Holle, alisema bado kuna taasisi za umma hazifanyi vizuri na kuzitaka zijitafakari ili zianze kufanya kazi kwa faida badala ya kutegemea ruzuku ya serikali.

"Tumekaa na Msajili wa Hazina na kumwelekeza afanye uchambuzi wa kina wa taasisi zinazotegemea ruzuku ya serikali kwa sababu ni jambo la aibu kwa kuwa taasisi zilianzishwa ili zitengeneze faida lakini bado zinategemea ruzuku kutoka serikalini," alisema.

Mkuu wa Mkoa Arusha, Paul Makonda, aliishukuru serikali kwa kutoa Sh. bilioni saba, kwa ajili ya kuboresha na kupanua uwanja wa ndege Arusha (Kisongo) kwa kuwa utawekwa taa ili kuziwezesha ndege kutua mchana na usiku.

"Hakuna uwanja wowote wenye ndege nyingi kama Arusha, hivyo kupanuliwa kwake kutaruhusu ndege nyingi zaidi kutua hapa na kupunguza foleni kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) wanazokumbana nazo baadhi ya watalii wanaokuja kutalii katika hifadhi zetu," alisema.

**Imeandikwa na Allan Isack, Cynthia Mwilolezi (ARUSHA)**




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akizungumza wakati akifungua kikao kazi cha Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma, jijini Arusha, jana. **PICHA: IKULU**

# Miili mingine 10 yabainika imefukiwa

**Na Romana Mallya**

UCHUNGUZI kuhusu matukio ya watu kutoweka umebaini mauaji mapya:

Katika kufuatilia mauaji yanayodaiwa kufanywa na mganga wa kienyeji na wenzake, Jeshi la Polisi limebaini miili mingine 10 ikiwa imefukiwa, baadhi imezikwa kwa mtindo wa kukaa, wakiwamo watoto wa watuhumiwa.

Jeshi la Polisi nchini limefafanua katika orodha hiyo mpya, wawili inadaiwa ni watoto, akiwamo wa mganga wa jadi na wanahisiwa walifukizwa wakiwa hai, matukio hayo yakichukua nafasi katika mikoa ya Singida (3) na Dodoma (7).

Katika mwendelezo wa matukio ya mauaji katika mikoa mitatu kuanzia mwishoni mwa wiki iliyopita, Msemaji wa Jeshi la Polisi, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) David Misime, alisema jana kuwa miili hiyo 10 ilibainika baada ya mahojiano na watuhumiwa.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, liliibuliwa sakata la matukio hayo ya mauaji katika mikoa hiyo ya Dar es Salaam, Tanga na Singida.

Kwa mujibu wa Misime, katika matukio mapya yalibainika mashimo mawili na yaliyofukuliwa na kupatikana mwili wa Gidion Mnyawi, mkazi wa Makuro, mkoani Singida.

Alisema Nkamba Kasubi, aliyemtaja kuwa ni mganga wa kienyeji, anadaiwa alielekeza Mnyawi atolewe kafara kutokana na kuuza shamba kwa watu wawili tofauti, kwa madai kwamba ndio njia ya kurejesha fedha zilizopotea.

DCP Misime alieleza kuwa katika shimo lingine, zilipatikana sehemu za mwili wa binadamu alizozitaja kuwa ni; nyonga, mikono ya kulia na kushoto.

Kamanda huyo alifafanua awali hawakugundua mwenye sehemu hizo za mwili, hata wakalazimika kuchukua hatua za uchunguzi zaidi, akifafanua:

"Baada ya uchunguzi huo na mahojiano ya kina na watuhumiwa ambao ni Selemani Nyalandu, maarufu Hango, Said Msanghaa, maarufu Mangu na Nkamba Kasubi..."

DCP Misime aliendelea: "Walieleza mwili huo ni wa Seleman Idd (23), mkazi wa Makuro Singida, ambaye walimuua kwa kumnyonga na kumfukia katika shimo Juni 23, 2024.

"Askari polisi wataalamu wa ufuatiliaji matukio makubwa walifanikiwa kupata taarifa kuwa kuna mtuhumiwa mwingine ambaye anaitwa Miraji Nyandalu, amehusika katika mauaji haya na wakafanikiwa kumkamata Agosti 25, 2024, huko katika Kijiji cha Misughaa, mkoani Singida.

"Alikuwa anajaribu kutoroka kwa kutumia pikipiki MC 262 CYU, mali ya Daudi Msanku ambaye walimuua na kumzika huko katika Kijiji cha Porobanguma, wilayani Chemba, Dodoma.

"Uchunguzi uliendelea na baada ya mtuhumiwa huyu (Nyandalu) kukamatwa na kukutanishwa na watuhumiwa wenzake, ndipo Nkamba Kasubi, mganga wa kienyeji, Agosti 27, 2024, alikubali kuwaongoza askari polisi hadi katika 'mji' (makazi) wake mwingine ulioko Kijiji cha Porobanguma, Tarafa ya Kwamtoro, wilayani Chemba na kuonesha mashimo sita ambayo walifukia watu wengine waliowaua na kuwazika (kuwafukia)," alisimulia.

"Daudi Msanku (27), mkazi wa Gawidu, mkoani Manyara ambaye alipotea Mei 27, 2024, na baada ya kumuua walichoma mwili wake moto kisha majivu yake kuyahifadhi katika ndoo, huyu ndiye ambaye pikipiki yake alikamatwa nayo Nyalandu akijaribu kutoroka baada ya kuona watuhumiwa wenzake wanakamatwa mfululizo na askari polisi," aliongeza.

DCP Misime alisema kuwa baada ya taratibu za ufukuaji kufanyika, ilipatikana miili ya watu wengine aliowataja ni; Seni Jishabi (28), mkazi wa Kijiji cha Porobanguma aliyepotea Machi 3, mwaka huu na watuhumiwa walidai kumuua na kumfukia mwezi uliofuata Aprili 2024.

Mwingine katika orodha ya waliouawa kwa mujibu wa polisi ni; Mohamed Juma (27), mkazi wa Nyamikumbi A, mkoani Singida aliyetoweka tangu Mei 15 mwaka huu ambao watuhumiwa wanadaiwa kumuua kwa kumnyonga kisha kumfukia.

DCP Misime alifafanua namna mauaji hayo yalivyohusisha wanafamilia wa watuhumiwa hao baadhi yao waganga wa kienyeji, akisema: "Ramadhan Yusuph (26), mkazi wa Kidika, mkoani Manyara, ambaye walimuua mwezi Aprili 2024; Mwekwa Kasubi (4), mtoto wa huyo mganga wa kienyeji; aliuawa Machi 2023.

"Maka Nyalandu (2), aliuawa Juni 2023, na ni mtoto wa mtuhumiwa Nyalandu, maarufu Hango. Watoto hawa walizikwa (walifukiwa) wakiwa hai katika zizi la mifugo.

"Pia, watuhumiwa walikiri kumuua Ramadhani Kilesa (80), mkazi wa Porobanguma na kutupa mwili wake katika Pori la Akiba Swangaswanga," alisema DCP Misime, aliyefafanua kuwa mwili wake ulipatikana Julai 25, 2024.

Alisema kuwa awali haikubainika wahusika tajwa wa mauaji yake hadi juzi (Agosti 27) wahusika walipokiri kumuua na kueleza sehemu walipomtupa ili mwili wake "uliwe na wanyamapori", lakini lengo lao halikutimia.

Kugundulika mauaji hayo ya watu 10 katika mikoa ya Singida na Dodoma, DCP Misime alisema unajumuisha utashi na imani hasi katika jamii.

"Hawa wote isipokuwa aliyetupwa katika Pori la Swangaswanga, kwani walibadili mbinu, tisa walizikwa (walifukiwa) kwa kukalishwa katika shimo kwa namna walivyosukumwa na imani zao za kishirikina," alisema.

DCP Misime alisema uchunguzi wa mlolongo wa matukio hayo ya Singida na Dodoma unaendelea, akiahidi polisi itafahamisha umma kadri taarifa mpya zitakapopatikana.

"Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa za kweli na sahihi na kuendelea kukemeana kuanzia ngazi ya familia ili kuzuia na kukomesha vitendo hivi vinavyoendelea kutokea ndani ya jamii kwa siri kubwa.

"Kila mmoja wetu tuelimishane kwa dhati, kwa kila mmoja kwa nafasi yake katika jamii ubaya na madhara ya kuendekeza imani za kishirikina, tamaa za mali bila ya kufuata maelekezo ya Mwenyezi Mungu, sheria za nchi na miiko katika jamii, kudhulumiana, kulipiza kisasi na wivu wa mapenzi," alisema.

## Makalla ataka kasi utendaji TPA

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla, ameuagiza uongozi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), kufanya kazi kwa kasi ili kuiwezesha Bandari ya Dar es Salaam kushika soko la biashara Afrika.

Pia amewataka kufanya kazi kwa kasi kwa kuhakikisha kunakuwapo na muungano kati ya bandari ya Dar es Salaam na Reli ya Kisasa (SGR) na kuzivutia nchi jirani.

Makalla alitoa maagizo hayo jana Dar es Salaam alipotembelea bandari hiyo kuona ufanisi na utendaji baada ya kufanyika uwekezaji.

"TPA chapeni kazi msirudi nyuma. Haya mnayoyafanya ni utekelezaji wa Ilani ya CCM. Msisikilize kelele za watu wala msitishike. CCM tunatembea kifua mbele tukiona maendeleo ya Bandari ya Dar es Salaam," alisema.

Makalla alisema wakati wa kutafuta wawekezaji wa bandari hiyo kulikuwapo na mjadala mkubwa na maneno kutoka kwa watu mbalimbali.

"Tuliokuwa tunajua nini kinaendelea kwenye uwekezaji ule wala hatukushangaa. Tulikuwa tunajua malengo na mipango ya serikali. CCM kazi yake ni kupanga na kuleta maendeleo kwa Watanzania bali wapinzani kazi yao ni kupinga," alisema.

Alisema vyama vya upinzani vimekuwa vikipinga miradi inayotekelezwa na serikali lakini ilikamilika wanakuwa wa kwanza kuitumia.

Akitolea mfano wa miradi hiyo, Makalla alisema: "Walipinga ununuzi wa ndege lakini leo wanapanda. Walipinga SGR leo tunapanda nao, walipinga mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere lakini leo wanafurahi tatizo la umeme kuisha. Kwa hiyo hatuwashangai wanapopinga hata uwekezaji Bandari ya Dar es Salaam."

Alisema kampuni ya DP World tangu iingie mkataba wa uendeshaji Bandari ya Dar es Salaam imeshatumia Sh. bilioni 214 kwa ajili ya uboreshaji wa vifaa, lengo lao ni kutumia Sh.bilioni 675.

Kwa muda wa miezi minne ya uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, alisema DP World imefanya maendeleo makubwa ikiwemo kuondoa msongamano wa meli zinazosubiri upakuaji.

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Juma Kijavara, alisema katika miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia mabadiliko makubwa ya kiutendaji yamefanyika katika Bandari ya Dar es Salaam.

Alitaja baadhi ya mafaniko hayo ni ukarabati wa magati, ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kushusha na kupakia mizigo. Mengine ni kupungua kwa siku za kushusha mizigo kutoka kwenye meli kutoka siku 20 za awali hadi siku saba.

Alitaja mafanikio mengine ni idadi ya mitambo ya kushusha na kupakia mizigo kuongezeka ambao umefanywa na DP World.

Kadhalika alisema mafanikio mengine ni ukarabati wa vifaa vibovu na kuanza kutumika tena kulikofanywa na DP World, ununuzi wa magari 20 ya kubeba mizigo.

Alitaja mafanikio mengine ni ununuzi wa jenereta mbili zenye ukubwa wa kv 10,000 zinazotumika kuendesha mitambo pindi umeme unapokatika.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe na wanachama wengine, wakiwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam jana, kusikiliza kesi ya wanachama wao, Deusdedit Soka na Jacob Mlay, wanaodaiwa kushikiliwa na polisi na kuomba waachiwe au wapewe dhamana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mahakama yaibana Polisi kupotea wakuu BAVICHA

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imelitaka Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi ili kujua waliko Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la CHADEMA (BAVICHA) Wilaya ya Temeke, Deusdedit Soka na Katibu wake, Jacob Mlay.

Mahakama imesema jeshi hilo linapaswa kufanya hivyo kwa sababu ndilo lenye jukumu la kulinda usalama wa raia na mali zake kama katiba na sheria zilivyoelekeza.

Pia mahakama imesema maombi yaliyowasilishwa mahakamani kuomba Soka, Mlay na dereva wa pikipiki, Frank Mbise, wanaodaiwa kuwa wako kizuizini, hayajathibitishwa kupitia kiapo kama ushahidi kwamba wanashikiliwa na jeshi hilo.

Jaji Wilfred Dyansobera alisema hayo jana wakati akitoa uamuzi juu ya maombi hayo huku akisema kiapo cha Mohamed Mzindu hakijathibitisha kama waleta maombi wako chini ya Mkuu wa Jeshi la Polisi.

Alisema hakijathibitisha kama raia hao wako chini ya Kamanda wa Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam (ZPC), Mkuu wa Upelelezi Kanda Maalumu Dar es Salaam (ZCO), Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Temeke (OC- CID) wala Mkuu wa Kituo cha Polisi Chang'ombe.

"Mahakama inaelekeza Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi kujua hawa waleta maombi wako wapi. Katiba na sheria imeelekeza kinagaubaga kuhusiana na jeshi kulinda usalama wa raia na mali zake.

"Haya maelekezo ninayoyatoa yanaendana na Sheria za Kimataifa ya mwaka 2010, sheria ambazo serikali inazifahamu kwa sababu na yenyewe iliweka saini. Hiki ninachokiagiza ni kusisitiza tu wajibu wa Jeshi la Polisi," alisema Jaji Dyansobera.

Jaji pia alisema wajibu maombi kupitia Wakili wa Serikali Mkuu, Jennifer Masue, kutaka kujua waliko waombaji, jeshi linatakiwa kufanya hivyo kwa sababu mahakama haiwezi kupuuza tuhuma za kutoweka kwa raia.

Alisema katika kiapo cha Mzindu ambaye alidai ni rafiki wa karibu wa waleta maombi (Soka, Mlay na Mbise) hakikuonesha kama alishuhudia waombaji kukamatwa na pia kwamba wako chini ya polisi.

"Yeye mwombaji anaamini kuwa wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa sababu Soka alimpigia simu kwamba anakwenda Kituo cha Polisi Chang'ombe kuchukua pikipiki akiongozana na Mlay na Mbise," alisema.

Jaji Dyansobera alisema mahakama haiwezi kutoa dhamana kama walivyoomba waleta maombi kwa sababu mtu aliyeachiliwa kwa dhamana bado yupo chini ya ulinzi, huwezi kumpa huru mtu ambaye anashukiliwa na polisi.

Pia alisema mahakama haiwezi kutoa amri waleta maombi waletwe mahakamani kwanza kwa mujibu wa kifungu cha 390 (1) (a) na (b) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) na kanuni kwa sababu haijulikani waliko.

"Kwa maombi yaliyoletwa kwa mamlaka niliyopewa polisi watekeleze wajibu wao. Mahakama inamatarajio makubwa polisi kufanya kazi waombaji wakapatikana,"alisema Jaji Dyansobera.

Wajibu maombi wengine katika shauri hilo, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG). Viongozi hao wa Bavicha wamekuwa hawajulikani waliko tangu Agosti 18, mwaka huu.

Kiapo cha Mzindu, kinadai kuwa siku hiyo Soka aliitwa kwa simu kwenda Kituo cha Polisi Chang'ombe kuchukua pikipiki yake ambayo ilikuwa inashikiliwa na tangu siku hiyo hawakuonekana tena wala kupatikana kwenye simu.

Kutokana na hali hiyo, Soka na wenzake kupitia kwa mawakili wao, wamefungua shauri la maombi wakiomba amri ya mahakama iwaamuru waachiliwe huru kutoka kizuizini au wajibu maombi wawafikishe mahakamani na kuendelea na taratibu nyingine za kisheria.

Waombaji hao wanawakilishwa na Wakili Peter Madeleka, anayesaidiana na mawakili Deogratius Mahinyila na Paul Kisabo. Walidai kwa mujibu wa Kanuni ya 7 ya Shauri la maombi ya aina hiyo, watuhumiwa waliowekwa kuzuizini huachiwa huru au kufikishwa mahakamani.

# Serikali yaja na marekebisho Sheria Ulinzi, Usalama Mtoto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kuwasilisha bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto, ili kukabiliana na vitendo vya ukatili vinavyoendelea nchini.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwantumu Zodo.

Mbunge huyo alitaka kujua upi mkakati wa serikali kukabiliana na vitendo vya ukatili vinavyoendelea nchini hasa kwa wanawake na watoto.

Naibu waziri alijibu kuwa muswada huo utasomwa katika mkutano huu wa Bunge kwa mara ya kwanza.

Aidha, alisema Mei 2024 imezindua Mpango Kazi wa Taifa wa awamu ya pili wa Kutokomeza Vitendo vya Ukatili kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA II).

Alitaja mikakati mingine kuwa ni elimu kwa umma imeimarishwa kwa ushirikiano na maofisa polisi ngazi ya kata pia, kimeanzishwa Kituo cha Huduma kwa Wateja wizarani ili kuongeza nguvu ya elimu kwa umma na kupokea taarifa za vitendo vya ukatili.

Alisema huduma za madawati ya Jinsia na Watoto zinapatikana katika vituo vyote vya Jeshi la Polisi pia, idadi ya vituo vya huduma ya dharura na jumuishi kwa manusura wa ukatili imeongezeka na kufikia vituo 26 nchini.

"Programu ya elimu ya malezi chanya, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto inatekelezwa kwenye mikoa na halmashauri zote nchini na kwa mwaka wa fedha 2023/24 wizara ilipata kibali cha ajira kwa maofisa maendeleo ya jamii 800 na maofisa ustawi 350," alisema.

# Polisi yazuia kigogo CCM kuzuru Ngorongoro

**Na Grace Mwakalinga**

JESHI la Polisi Wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha limezuia Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM ), Amos Makalla kuzuru wilayani humo kutokana na linachoeleza kuwa "sababu za kiusalama".

Imeelezwa kuwa kigogo huyo wa CCM alitarajiwa kufanya ziara wilayani Ngorongoro Septemba 6 mwaka huu na kufanya mikutano ya kisiasa kuanzia saa nne asubuhi hadi saa 11 jioni.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Polisi Wilaya ya Ngorongoro, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP) Leah Ncheyeki, walipokea barua juzi kutoka CCM yenye kumbukumbu namba CCM/NGN/OFU/10/311/VOLI11/37 ya tarehe 23 Agosti mwaka huu kuomba kibali cha kufanya mikutano hiyo.

Alisema barua hiyo ilikuwa na maelezo kutoka CCM kuomba kibali cha kufanya mikutano ya hadhara ya Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo (Makalla) wilayani Ngorongoro.

"Kutokana na shughuli za kuimarisha usalama zinazoendelea katika maeneo mliyoomba kufanyia mikutano, tunawajulisha kuwa tumesitisha mikutano, mikusanyiko ya watu katika maeneo hayo hadi tutakapoelekeza vinginevyo," inaelezwa katika barua hiyo ya Mkuu wa Polisi Wilaya ya Ngorongoro.

Hii si mara ya kwanza Jeshi la Polisi kuzuia mikutano ya kisiasa kufanyika wilayani Ngorongoro. Septemba 9 mwaka jana, viongozi na wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) walizuiwa na polisi kuingia ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA).

Viongozi hao wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu walizuiwa kuingia ndani ya eneo hilo kufanya mkutano wa hadhara kutokana na kilichoelezwa na jeshi hilo kuwa "sababu za kiusalama".

Mkuu wa Polisi Wilaya ya Ngorongoro, (wakati huo ACP Peter Lusesa), alikiandikia barua chama hicho kuzuia mikutano kiliyopanga kufanya wilayani humo kwa madai ya "sababu za kiusalama katika eneo la Loliondo na Ngorongoro".

Mjumbe wa Kamati ya Utendaji CHADEMA Wilaya ya Karatu, Joseph Mtui, alisema wakiwa wameambatana na viongozi wa kitaifa kwenda Ngorongoro, walizuiwa na polisi.

Alisema kuwa kabla ya kuanza safari, walipewa taarifa kwamba wanatakiwa kuwa na vibali vya kuingia hifadhini na walianza taratibu za kuvipata lakini baadaye walipata taarifa ya kuzuiwa wakati tayari viongozi wakiwa eneo la kituo cha ukaguzi wa watalii.

Vilevile, Juni 20 mwaka huu, Jeshi la Polisi lilizuia mkutano wa CHADEMA kufanyika katika Tarafa ya Ngorongoro, likiwa na maelezo kuwa taarifa za kiintelijensia zilionesha si salama kwa wakati huo kufanya shughuli za kisiasa katika eneo hilo.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (katikati), akiangalia mifugo katika Kijiji cha Mpelumbe, Kata ya Gwata, wilayani Kibaha, mkoani Pwani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafugaji Pwani waitika wito ufugaji kisasa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewapongeza wafugaji wa Kijiji cha Mpelumbe, Kata ya Gwata, wilayani Kibaha, mkoani Pwani kwa kujitolea kujenga bwawa la kunyweshea mifugo yao.

Waziri Ulega alitoa pongezi hizo hivi karibuni wakati alipowatembelea kuona juhudi wanazozifanya ambazo zinaunga mkono jitihada za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan za kuboresha sekta ya mifugo ili iwe na mchango mkubwa kwa taifa na mtu mmoja mmoja.

"Nawapongezeni sana, na nitakwenda kumjulisha Mheshimiwa Rais kuhusu jitihada zenu hizi, kwa kweli mmefanya kazi nzuri sana na sisi wizara tunakwenda kuwaweka katika mipango yetu kuanzia mwezi wa 12 hadi wa kwanza mwakani tutawapatia Sh. milioni 50 ili ziwasaidie kuboresha bwawa hili mliloanza wenyewe kulitengeneza," alisema.

Aidha, Waziri Ulega aliwaelimisha kuhusu Kampeni ya TUTUNZANE iliyozinduliwa na Rais Samia mkoani Morogoro inayohamasisha ufugaji wa kisasa ikiwamo kulima malisho, kuchimba mabwawa na kutunza mazingira.

Aliwahimiza wafugaji hao kuwa na maeneo yao kwa ajili ya kulima malisho aina ya Juncao kwa ajili ya mifugo yao huku akiwakabidhi mbegu aina ya rhodes ili wapande katika maeneo yao.

Waziri Ulega alimpongeza Mfugaji wa Kijiji cha Gumba, Kata ya Gwata, wilayani Kibaha, mkoani Pwani, Muhammadi Ragwa, kwa jitihada aliyoifanya ya kuacha ufugaji wa asili na kufanya ufugaji wa kisasa wa kunenepesha mifugo ambao umemwezesha kupiga hatua kubwa.

Alimtembelea hivi karibuni mfugaji huyo katika eneo lake la ufugaji na kujionea maendeleo mbalimbali aliyoyafanya ikiwamo kujenga bwawa la kunyweshea mifugo yake, kujenga maghala ya kuhifadhia chakula cha mifugo na mashine ya kuchakata chakula cha mifugo yake.

Alisema hiyo ni hatua kubwa kwa kuwa anachokifanya ndio mwelekeo ambao serikali inataka wafugaji kote nchini kuuchukua, inahimiza wafugaji kubadilika kutoka katika ufugaji wa asili na kufanya ufugaji wa kisasa ikiwamo kuwa na maeneo yao ya kufugia.

Kutokana na maendeleo makubwa aliyoyaona kwa mfugaji huyo, Waziri Ulega amempatia mbegu za malisho na pia amewaelekeza wataalamu kutoka wizarani kwake kuhakikisha wanajenga josho katika kijiji hicho ambalo litasimamiwa na Muhammadi kwa niaba ya wafugaji wote ikiwa ni kama motisha kwa mfugaji huyo na wengine pia.

"Ile mipango mizuri ya Rais Dk. Samia ya kuboresha sekta ya mifugo inapaswa ielekezwe katika maeneo kama haya ya wafugaji walioipiga hatua kama Muhammadi kwa sababu inakuwa katika mikono salama," alisema.

Akitoa taarifa fupi ya historia ya ufugaji wake, Muhammadi alisema kiasili amezaliwa kwenye familia ya kifugaji na alirithi mtindo wa ufugaji kutoka kwa wazee wake ambao ni wa kuhamahama kutafuta maji na malisho.

Baada ya kupata changamoto nyingi zilizotokana na ufugaji wa kuhamahama ikiwamo magonjwa kwa mifugo aliamua kuacha mfumo huo na kuanza ufugaji wa kisasa wa kuinenepesha ambayo umempatia manufaa makubwa ikiwamo kuwa na makazi ya kudumu ya familia yake na mifugo yake, kujenga miundombinu ya kufugia mifugo ikiwamo lambo la kunyweshea, maghala ya kuhifadhia chakula cha mifugo na mashine ya kuchakata chakula cha mifugo.

SAKATA LA WODI

# Spika Tulia aagiza mbunge awasilishe ushahidi bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amemwagiza Mbunge wa Ilemela (CCM), Dk. Angelina Mabula kuwasilisha bungeni kesho ushahidi kuhusu madai ya Kituo cha Afya Sangabuye, Manispaa ya Ilemela, mkoani Mwanza kuwalaza katika wodi moja wanaume, wanawake na watoto.

Akitoa maelekezo hayo jana baada ya kipindi cha maswali na majibu, Spika Tulia alisema: "Jana (juzi) katika majibu ya serikali kulikuwa na hoja ya Kituo cha Afya Manispaa ya Ilemela na nilimwagiza mbunge alete ushahidi kwa namna kanuni zetu zinavyotaka, lakini nilikuwa sijampa tarehe ya kuleta huo ushahidi. Sasa nimpe tarehe ya kuleta itakuwa Agosti 30, 2024."

Suala hilo liliibuliwa bungeni juzi baada ya mbunge huyo katika swali la nyongeza kulieleza Bunge kuwa kituo hicho kimetokana na kupandishwa hadhi zahanati iliyokuwapo kuwa kituo cha afya mwaka 1999, lakini hadi sasa kina wodi moja inayotumiwa na wanawake, wanaume na watoto.

Mbunge Angelina pia alihoji lini serikali itakamilisha majengo ya kituo hicho pamoja na kujenga uzio.

Kabla ya kumkaribishwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, kujibu swali hilo, Spika Tulia alionesha shaka kuhusu jambo hilo na kumhoji mbunge huyo, "wanalalaje katika hiyo wodi yenye watoto, wanawake na wanaume?"

Mbunge alimwambia Spika kuwa ni kweli wanatumia wodi moja na Spika akahoji tena wanawezaje kulala wodi moja, akionesha shaka na kuhoji tena wameweka mapazia au la.

Akifafanua, Mbunge Mabula alisema katika kituo hicho cha afya, wodi hiyo ina kitanda kimoja analazwa mwanamke na kinachofuata kuna mwanaume na kingine kuna mwanamke na mtoto na ni tangu 1999 miundombinu haijakamilika.

Akijibu swali hilo la nyongeza, Naibu Waziri Dugange, alisema kwa mujibu wa utaratibu na Sera ya Afya, hairuhusiwi kulaza wagonjwa wa jinsia tofauti katika wodi moja.

"Kwa taarifa hii, TAMISEMI tunaipokea kwamba kuna tatizo katika uongozi wa hospitali hiyo na manispaa yenyewe, naomba mheshimiwa Spika nichukue hoja hii nimwelekeze Mkurugenzi wa Manispaa leo hii afike pale mara moja na atupe taarifa rasmi TAMISEMI ili kuona namna nzuri ya kutoa huduma kwa wagonjwa wanaolazwa kwa kuwa haikubaliki kulaza wanawake na wanaume wodi moja," alisema.

Naibu Waziri huyo pia aliagiza Mkurugenzi wa Manispaa hiyo kupitia mapato ya ndani kuanza ujenzi wakati TAMISEMI ikitafuta fedha kwa ajili ya kuwaunga mkono.

Hata hivyo, Spika Tulia alielekeza TAMISEMI itafute taarifa kwa kina kuhusu suala hilo na kutolea ufafanuzi bungeni ili kueleza watu hao wanalalaje katika wodi moja na kuliweka sawa jambo hilo katika taarifa za Bunge.

## ERB yatoa ufadhili walimu 20 kufundisha masomo ya sayansi

**Na Joyce Lameck**

BODI ya Usajili wa Wahandisi (ERB) imepeleka walimu 20 wa masomo ya Fizikia na Hisabati katika shule tatu, ili kusaidia serikali kuongeza idadi ya walimu wa masomo hayo na kuongeza mwamko wa wanafunzi kuyapenda.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi mkoani Dar es Salaam, Msajili wa Bodi hiyo, Bernard Kavishe, alisema lengo ni kupeleka takribani walimu 100 wa kujitolea katika shule 26 nchini ambao watagharamiwa na ERB.

Kavishe aliomba wadau kuunga mkono mbio za marathon zinazotarajiwa kufanyika Dar es Salaam Septemba 6, mwaka huu, kwa ajili ya kupata fedha za kulipa posho walimu wa kujitolea wa masomo ya sayansi katika shule mbalimbali nchini.

Alisema mgeni rasmi katika mbio hizo anatarajiwa kuwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda.

"Hadi sasa walimu 20 wanafundisha katika shule tatu za mikoa ya Kagera, Geita na Dar es Salaam. ERB inawagharamia posho, nauli na bima ya afya," alisema.

"Tulifanya utafiti na kubaini kuwa tunapaswa kuandaa wataalamu kuanzia ngazi za chini kabisa.

"Tulibaini kuna upungufu wa walimu wa Fizikia na Hisabati. Tumekuja na mpango wa kutafuta fedha za kugharamia walimu wa kujitolea. Tunaunga mkono jitihada za serikali kuhakikisha walimu wanakuwapo wa kutosha," alisema.

Kavishe aliomba wadau kujitokeza kuwaunga mkono jitihada hizo ili kupata fedha za kugharamia walimu zaidi watakaokwenda kufundisha masomo hayo katika shule ambazo wamezitambua.

Alisema serikali imejenga miundombinu ya elimu katika ngazi mbalimbali na kutoa nafasi kwa wadau kugharamia walimu wa kujitolea, hivyo wanasaidia kuandaa wahandisi tangu ngazi za awali.

Kavishe alisema mbio hizo zitatanguliwa na kongamano la vijana katika tasnia hiyo litakalofanyika kwa siku mbili kuanzia Septemba 3 mwaka huu, ambalo pamoja na mambo mengine, wataeleza umma ni kwa namna gani wanafanya kazi zao.

Alisema Septemba 5, mwaka huu, kutafanyika kongamano lingine litakalojumisha takribani watu 6,000, kati ya hao wahandisi watakuwa 4,000.

# Wamiliki shule binafsi waeleza mkwamo utekelezaji Bima ya Afya kwa wanafunzi

**Na Jenifer Gilla**

WAMILIKI wa shule binafsi wamesema utekelezwaji wa huduma ya utoaji Bima ya Afya kwa watoto kupitia shuleni iliyoelekezwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umekuwa mgumu kutokana na wazazi wengi kugoma kuandikisha watoto wao.

Walisema sababu kuu ya wazazi kuikataa ni wengi wao kuwakatia kupitia kwenye ajira zao na baadhi wakiulalamikia mfuko huo kutokuwa na huduma za kuridhisha.

Mmiliki wa Shule ya Sekondari ya Lake iliyopo mkoani Arusha, Leonard Mao, alisema walisikia taarifa hiyo kupitia vyombo vya habari na walipojaribu kutoa taarifa kwa wazazi utekelezaji wake umekuwa mgumu.

Alisema watoto wengi wanaosoma shuleni hapo wazazi wao ni wafanyakazi wa serikalini na binafsi ambao wamewakatia bima ya afya kupitia maeneo yao ya kazi na kwamba walikataa kuwakatia bima nyingine kupitia shuleni.

"Kwa hiyo bima ya mzazi wake aliyokuja nayo utaiondoa ili umpe nyingine? Watoto wengi wanaosoma hapa wazazi wao ni watumishi ambao kwa asilimia kubwa wana bima," alifafanua.

Aidha, alishauri mfuko huo kutafuta utaratibu mwingine wa kuwakatia watoto hao bima, kwa kuingia makubaliano na wazazi wao moja kwa moja kupitia maeneo wanayofanya kazi au kwenye biashara zao.

Mao ambaye ni Mwenyekiti wa Taifa wa Shirikisho la Wamiliki wa Shule na Vyuo Binafsi Tanzania (TAMONGSCO), alisema wanatarajiwa kufanya kikao na wamiliki wa shule binafsi na kuandika mapendekezo yao na kuyapeleka NHIF.

> **"Kwa hiyo bima ya mzazi wake aliyokuja nayo utaiondoa ili umpe nyingine? Watoto wengi wanaosoma hapa wazazi wao ni watumishi ambao kwa asilimia kubwa wana bima,"**

Ofisa Mtendaji Mkuu Taasisi ya Ubunifu Katika Elimu (EIT), Benjamin Mkonya, alisema walipokea barua hiyo kutoka NHIF, lakini walipopeleka hoja hiyo kwa wazazi waliikataa kwa madai ya kuwa mfuko huo ni dhaifu katika huduma ya matibabu.

Alisema wazazi wengi walikuja na hoja kuwa unapokwenda hospitali kutibiwa na kadi ya mfuko huo hawapati huduma nzuri, ikiwamo kukataa kuhudumia baadhi ya vipimo na hawapati dawa muhimu.

Alisema wengi wa wazazi walisema kuwa wamehama kutoka mfuko huo na kuhamia mingine ili watoto wao wapate huduma stahiki na wasingependa kurudi huko mpaka watakapojiridhisha kuwa umeboreshwa.

"Wazazi walisema hawaitaki kwa sababu ya upatikanaji wake wa matibabu ni wa shida kwa maana ya kuwa hata baadhi ya dawa hazipatikani kupitia mfuko huo," alisema.

Mmliki wa Shule ya Msingi ya Uhuru Peak iliyopo Ngurelo, mkoani Arusha, Girbert Sarungi, alisema bado hajaanza kutekeleza suala hilo kwa sababu hajapewa utaratibu wa namna ya kutekeleza kutoka kwa NHIF.

Sarungi ambaye ni Mwenyekiti wa Wamiliki wa Shule Binafsi Mkoa wa Arusha, alisema walisikia taarifa kuwa utaratibu wa kutoa bima za afya kwa watoto utafanyika kupitia shule, lakini bado NHIF haijakaa nao rasmi na kuwaelekeza ni kwa namna gani watakuwa wanapeleka makato hayo.

"Basi sijafahamu kuwa mchango utatolewa kwa namna gani, kama nitamkata mzazi kwenye ada au la, kwa hiyo hata wazazi wenyewe bado sijawaeleza suala hili mpaka pale mfuko (NHIF) utakaponipa maelekezo," alisema.

Mmiliki wa Shule ya Sekondari Vanessa, iliyopo Mbeya Mjini, Mkoa wa Mbeya, Shukrani Gideoni, anaungana na hoja na mtangulizi wake kuwa alisikia kuanzishwa kwa huo utaratibu kama watu wengine lakini.

Mmoja wa wazazi, Angela James, alisema licha ya kuwa mpango huo ni mzuri kwa wanafunzi hawezi kumkatia mtoto wake huduma hiyo kupitia shule kwa sababu alishamuunganisha kupitia kazini kwake.

Alisema huduma hiyo inafaa zaidi kwa wafanyabiashara au wazazi ambao hawawezi kuifikia huduma hiyo na kuishauri NHIF kuruhusu wamiliki wa shule kuwakatia bima watoto ambao wanaihitaji.

Nipashe iliwatafuta NHIF kwa ajili ya kufafanua hoja za wamiliki na wakuu hao wa shule kwa takribani wiki nmoja bila mafanikio baada ya Kaimu Meneja Uhusiano, Grace Michael, kutoa taarifa kuwa Mkurugenzi Mkuu, Irene Isaka yupo kwenye vikao, lakini baadaye simu yake ilivyopigwa haikupokewa.

Septemba 23, mwaka jana aliyekuwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alisema kuwa serikali imebadilisha utaratibu wa kuwasajili watoto katika Mfuko wa Bima ya Afya na watapata huduma hiyo kupitia shuleni kwa gharama ile ile ya Sh. 50,400.



Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara, Remidius Mwema, akishiriki kuchimba msingi alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa shule mpya ya sekondari Kata ya Makame juzi, ambapo serikali imetoa Sh. milioni 584. **PICHA: GIFT THADEY**

# Watumishi wapewa vibali kufuata wenza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2023/24, vibali vya uhamisho wa watumishi 8,846 vimetolewa, wakiwamo wanaowafuata wenza wao.

Hivi sasa serikali inafanya tathmini ya hali ya mahitaji ya watumishi na baada ya kukamilika itajua mahitaji halisi na kufanya msawazo katika maeneo ambayo yatakuwa na upungufu.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, aliyasema hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ng'wasi Kamani.

Mbunge huyo alitaka kujua mkakati wa serikali kuendeleza ustawi wa familia kwa kuweka wanandoa waajiriwa katika vituo vya kazi vya karibu.

Akijibu swali hilo, Sangu alisema tathmini hiyo itasaidia pia kujaza nafasi katika maeneo yenye upungufu uliotokana na wanandoa waliofuata wenza wao.

"Serikali inatambua na kuthmini ustawi wa familia ambao ni muhimu kwa ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla. Na kwa msingi huo, imeweka kipindi cha chini kwa mtumishi kukaa katika kituo kimoja cha kazi kabla ya kuhamishwa kuwa ni miaka mitatu," alisema.

Alisema kuwa baada ya kipindi hicho kupita, watumishi wanaweza kuwasilisha maombi ya uhamisho kwenda maeneo mengine kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kuungana na wenza wao.

Hata hivyo, alisema maombi hayo yanapaswa kuzingatia kuwapo mahitaji ya rasilimali watu kwa kada husika katika maeneo hayo.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua ya kufutwa mashirika mzigo kwa serikali inastahili kupongezwa

**SERIKALI** kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imekuwa katika mpango wa kuboresha utendaji wa mashirika na taasisi za umma ili kuleta ufanisi katika utendaji wao wa kazi na hatimaye kuleta tija na kuchangia pato la taifa.

Katika kutimiza azma hiyo, serikali imekuwa ikisisitiza kuwa mashirika na taasisi hizo zinapaswa kufanya kazi kwa ubunifu ikiwamo kujiendesha kwa faida badala ya kutegemea ruzuku kutoka serikali kuu kwa ajili ya uendeshaji na kulipa mishahara wafanyakazi. Mbali na kufanya hivyo, yanapaswa kupeleka gawio serikalini.

Huku yote hayo yakisisitizwa, kwa takribani miaka mitatu sasa, Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akiagiza bodi za wakurugenzi chini ya wenyeviti wao na watendaji wakuu wa mashirika na taasisi hizo, wanapaswa kuwa wabunifu na kwamba ufanisi katika utendaji kitaguwa kigezo cha kuendelea kuwa katika nafasi hizo au la.

Wakati wa maandalizi ya kongamano la wenyeviti na watendji wakuu wa mashirika na taasisi za umma lililoanza jana jijini Arusha, Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, juzi alitangaza kuwa serikali imeanza kutekeleza azma ya kuyafuta mashirika na taasisi ambazo ni tegemezi kwa serikali. Katika kufanya hivyo, Mchechu alisema kwa mwaka wa fedha wa 2024/25, serikali inatarajia kuzifuta taasisi na mashirika ya umma takriban 40 yaliyoshindwa kujiendesha, hivyo kutegemea ruzuku na gharama za uendeshaji kutoka serikali kuu.

Kwa mujibu wa Mchechu, lengo la kufanya hivyo ni kuwa na taasisi ambazo zinatoa mchango kwa pato la taifa na zile ambazo zinafanya vibaya ikiwa ni pamoja na kutegemea ruzuku kwa serikali kwa uendeshaji na kulipa misharara ya wafanyakazi, zitafutwa ili kuiondolea mzigo serikali.

Kwa sasa serikali ina mashirika ya taasisi za umma 248 pamoja na zingine 58 ambazo zinamiliki asilimia 50 kushuka chini, hivyo kuna ulazima mkubwa wa kufanya ukaguzi ili kuona kama yote hayo yana tija kwa serikali au la. Kwa uamuzi wa serikali wa kuyafuta inamaanisha kwamba yako mashirika na taasisi mzigo ambayo yanapaswa kufutwa au kubinafsishwa.

Uamuzi wa serikali wa kufuta taasisi hizo ambazo ni mzigo ni wa kuungwa mkono kwa sababu fedha zinazotumika kuyaendesha zingetumika kufanya majukumu mengine na kuondoa kero zinazowakumba wananchi kama maji, barabara, elimu na afya. Ni afadhali kuwa na taasisi chache zenye uwezo na kuleta tija na ufanisi na wakati huo huo kupongeza pato la serikali.

Kama alivyoagiza Rais Samia kwa watendaji na wenyeviti wa bodi za wakurugenzi kuhusu ubunifu, inaonesha wazi kwamba mashirika na taasisi hizo ambazo ziko katika mchakato wa kufutwa, waliopewa dhamana wamekosa ubunifu au kuwa na mikakati ya kuyaendeleza. Hadi kufikiwa kwa hatua hiyo, kunadhihirisha kwamba wataacha alama hasi kiutendaji na pia itasababisha wafanyakazi wa taasisi hizo kupoteza ajira.

Kuna msemo kwamba mwenzio akinyolewa tia maji. Kwa msemo huo, mashirika yatakayokwepa mtego wa kufutwa yanapaswa kujitafakari kama hayatafuata awamu ijayo kwa hatua kama hiyo. Ni wajibu wa bodi, menejimenti na wafanyakazi kuhakikisha wanafanya kila liwezekanalo ili kubaki kwenye orodha ya msajili na dawa pekee ni kuwa wabunifu.

Watu hao waliopewa dhamana ya kusimamia taasisi na mashirika hayo, wanapaswa kujiuliza imekuwaje wengine wakafanikiwa kuyafanya mashirika na taasisi zao kufanya vizuri na wao washindwe?

Ni dhahiri kwamba hakuna muujiza wowote uliowafanya kufanikiwa na taasisi zao kuwa kielelezo cha ufanisi na mafanikio zaidi ya kuwa wabunifu na kutekeleza mipango na mikakati waliyojiwekea katika kufikia malengo na mafanikio ya taasisi hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Polisi iwashe tochi yake kumulika wanaoichafua

Na Beatrice Moses

**NAWAKUMBUSHA** Jeshi la Polisi kwamba lengo lao linajulikana kuwa ni kutoa huduma bora zitakazowezesha kubaini, kuzuia na kudhibiti uhalifu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Linapotimiza wajibu wake, ni wazi kuwa hakuna maneno ya kuwashangilia japo pongezi ni muhimu zinatia moyo.

Hadi sasa, Polisi wanawajibika katika kulinda usalama wa raia na mali zao imani ya wananchi imejengwa hivyo. Kwa hiyo, inapotokea tofauti, ndipo yanapoibuka maneno ya kulishambulia na malalamiko mengi dhidi yake, kwa kuwa linatazamwa kama vile limeshindwa kutimiza wajibu wake kwa wananchi.

Inawezekana, kuna watu wana hulka ya kulalamika, lakini ukweli unabaki kuwa ukweli, kama msemo wa wahenga usemao "palipo na ukweli uongo hujitenga." Kwa hiyo, kuna haja ya jeshi hilo kujitathimini mara kwa mara ili kuendelea kujijengea imani kwa wananchi.

Awali askari polisi waliaminika na kuogopwa na wahalifu, lakini hali imebadilika kwa kiasi, wakati huu kwa kuwa kuna polisi kadhaa waliobainika kushiriki kwenye uhalifu, ikiwamo kupora mali waliopaswa kulinda, wengine kujikwapua vidhibiti (ushahidi) kujimilikisha isivo halali.

Viongozi wa jeshi hilo, wana kazi kubwa ya kuwabaini mapema askari wao wenye mwenendo potofu. Polisi mmoja anapobainika kujihusisha na uhalifu, kwa hakika analichafua jeshi zima na ama analipunguzia au kuoondolea uaminifu kwa wananchi, hivyo kusababisha chuki.

Hilo la chuki ni hatari na tishio la aina yake pale, kwa kuwa imethibitika pale baadhi ya wananchi walipoonyesha hisia zao za kufurahi polisi walipokumbwa na mabaya. Binfasi, sitaki kuwatonesha kidonda kwa kutaja matukio hayo ya huzuni yaliyotokea miaka kadhaa iliyopita.

Kwani upande mmoja unajulikana, wahalifu hawawezi kulipenda kwa kuwa linawaharibia au inawazuia kufanya uovu wao hivyo wasingependa kuliona, raia wema wao moja kwa moja wanawapenda polisi kwa kuwa uwepo wao unawafanya wawe salama na mali zao.

Daima ukweli huwa ni mchungu, lakini ilitegemewa matukio kadhaa mabaya yalivotajwa kuwahusisha baadhi polisi yangeweza kutoa nafasi kwa Jeshi la Polisi kujitathimini na hata kuwasha tochi zao mara kwa mara kujimulika, hasa kwenye utendaji wao.

Hapo ni kuwabaini na hata kuwanyofoa mapema wenye tabia ovu, kabla hawajazama kutenda uovu wao na kulipa jeshi hilo wakati mgumu.

Mfano kuna hili jambo nimewahi kulisikia kwamba "kuingia polisi ni bure lakini kutoka lazima kutolewe chochote" Je viongozi wakuu wa jeshi hili wamelifuatilia hilo kwa kiasi gani ili kuwathibitishia raia kuwa hili jambo halipo bali jeshi linafanya kazi zake kwa msingi na taratibu za sheria zilizopo.

Ni wazi kuwa yapo mazuri mengi ambayo yanaonyesha jinsi polisi waavyowajibika ipasavyo, lakini huwa hakuna pongezi nyingi kama ilivyo kwenye malalamiko, kwa sababu inatarajiwa jeshi hilo kufanya vizuri ndiyo ni wajibu wake.

Polisi inanyooshewa kidole na taasisi zinazoaminiwa na wananchi, kama vile Baraza la Uongozi wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), ambayo kupitia taarifa yake, ilidai kuwa watu 83 baadhi yao wamepotea, wametekwa na kuteswa na wakalaani hayo. TLS ambao ni mkusanyiko wa wasomi wa sheria, wanaojua kuchambua sheria, kulingana na vigezo vinavyostahili, imelinyooshea kidole jeshi hilo kwamba limekuwa na tabia ya kukanusha taarifa za matukio kadhaa lakini baadaye ukweli hubainika.

Mnamo Agosti 22 mwaka huu, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (TBUB), ilitangaza kufuatilia matukio ya utekaji watu wanaopotea katika mazingira ya kutatanisha.

Hivi karibuni, jeshi hilo lilitangaza nafasi za ajira kwa wenye elimu na kada tofauti, zikiwamo ngazi za shahada, stashahada na astashahada, pia kidato cha nne.

Najua siyo mara yao ya kwanza kutangazwa nafasi hizo za ajira, lakini ni vyema nafasi hizo zingetumika katika kulisuka na kuliimarisha jeshi hilo kuwa la kisasa linalokwenda na teknolojia maana uhalifu wa kisasa nao unashika kasi. Hivyo, damu changa hiyo inapoingizwa kwenye mfumo wa ajira wa jeshi hilo itarajiwe kuonekana utendaji wenye mabadiliko kwa siku zijazo, ambao pia utasaidia kupunguza lawama kwa jeshi hilo.

## HABARI KITAIFA

## Mpango: NMB ieneze elimu ya bima kwa watumiaji wa vyombo vya moto

**Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango ameitaka Benki ya NMB kuwafikia watu wengi zaidi kwa ajili ya kuwapa elimu ya bima, hasa waendeshaji na watumiaji wa vyombo vya moto.

Dk. Mpango alitoa kauli hiyo juzi alipotembelea banda la maonesho la NMB katika maadhimisho ya miaka 50 ya Baraza la Taifa la Usalama Barabarani ambapo kilele chake kilifanyika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma.

Benki ya NMB kwa kushirikiana na kampuni za Bima za Sanlam na Reliance walikuwa wadhamini wakuu kwenye maadhimisho hayo huku ikiwa ni mwaka wa tatu mfululizo kwa benki hiyo kuwa mdhamini mkuu wa maadhimisho hayo.

Makamu wa Rais amesema suala la Bima kwa watumiaji wa vyombo vya moto ni muhimu lakini watu wengi hawana elimu ya kutosha kuhusu umuhimu huo jambo alilosema NMB inao uwezo wa kuwafikia Watanzania wengi na kwamba inaaminika.

"Watu wengi hawaoni thamani ya bima, mtu akikata bima mwaka wa kwanza hadi miaka minne anaona hakuna tatizo basi anaacha, ninyi NMB mnaweza kuifanya kazi hiyo vizuri, niwatake mkaifanye kwani kinga ya chombo cha moto ni bima na si vinginevyo," aliagiza Dk. Mpango.

Alisema kuwa, baadhi ya watu wanaona bima inanufaisha benki na kampuni za bima wakati si kweli, hivyo akaomba elimu zaidi ipelekwe hasa kwa waendesha pikipiki maarufu bodaboda ili wajiunge na kusema NMB ni mahali sahihi kufanya hivyo.

Mkuu wa Idara ya Bima kwa Benki ya NMB, Martin Massawe, alisema ndani ya benki hiyo kuna mfumo wa kuwawezesha watumiaji wa vyombo vya moto kukata bima kwa gharama ndogo inayobebeka.

Massawe alisema benki hiyo inatoa bima hadi ya Sh. 200 kwa mwezi huku watumiaji wa vyombo vya moto wakitakiwa kukata bima ya kuanzia Sh. 10,000 kiasi ambacho kinawezekana kwa kundi hilo kwa kumudu kulipia.

Kwa mujibu wa Massawe, NMB imefanya mazungumzo na viongozi wa madereva nchini ambapo mwikitio ni mzuri kwa kuwa wengi wameshajiunga na kukata bima za vyombo vyao na bima za maisha yao, lakini akakiri kupokea maagizo ya kuongeza nguvu katika utoaji elimu zaidi. Akitoa salama kwa niaba ya wadhamini wengine, Massawe alisema Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani wameipa kipaumbele na ndiyo maana wamebeba jukumu la udhamini kwa mwaka wa tatu.

Massawe aliomba Watanzania na wakazi wa Dodoma kutembelea matawi ya NMB maeneo yote ili wapate fursa nyingi, ikiwamo mikopo kwa ajili ya vyombo vya moto na biashara kwa masharti rafiki ambayo benki inazingatia kwa maisha ya wananchi.




Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Foundation for Disabilities Hope, Michael Salali (kulia), akizungumza wakati akiutambulisha mradi wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto wenye ulemavu, uliofadhiliwa na Taasisi ya Women Fund Tanzania Trust, katika kijiji cha Buigiri, wilayani Chamwino, mkoani Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC aonya kinamama kutetea watuhumiwa ukatili wa kijinsia

**Na Halfani Chusi,** KONDOA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amesema kukwama kwa kesi nyingi za ukatili wa kijinsia katika mkoa huo kunatokana na baadhi ya kinamama kuwatetea watuhumiwa.

Vilevile, amesema mkoa huo una changamoto ya vifo vingi vinavyosababishwa na wivu wa mapenzi na ulevi uliopitiliza.

Kiongozi huyo aliyasema hayo juzi wilayani Kondoa wakati wa Tamasha la Saba la Jinsia ngazi ya wilaya linalolenga kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 20250 na miaka 30 ya mkutano wa Beijing.

Rosemary alisema kuwa katika kushughulikia kesi hizo, walibaini kinamama wanatumia nguvu kubwa kutetea watu waliofanya ukatili badala ya kutumia nguvu hiyo kuzuia vitendo hivyo.

"Tabia hii katika mkoa huu imekuwa kikwazo katika kukabiliana na matukio ya ukatili ambayo asilimia 60 yanaanzia majumbani.

"Tujenge maadili katika nyumba zetu kwa kukemea na kuonya watu kabla ukatili haujafanyika. Suala la maadili si la mwalimu peke yake, wazazi pia wanatakiwa kupinga ukatili kuanzia nyumbani," alisema.

Kutokana na hali hiyo, kiongozi huyo aliagiza halmashauri zote za mkoa huo kuendelea kutoa elimu za masuala ya ukatili na namna ya kuyakabili pamoja na kuhamasisha wananchi kutoa maoni yao kuhusu Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050.

Pia alizitaka halmashauri kufanya kampeni ya kuwaeleza wanakondoa fursa zilizoko serikalini, akionya kutofanya hivyo ni kumnyima mwananchi fursa zilizoko. "Vifo vingi Dodoma vinasababishwa na ulevi na wivu wa mapenzi, ulevi tunaweza kuzuia kwa sababu watu wanaanza kunywa mapema kinyume cha muda wa serikali.

"Watendaji wa vijiji, kata mpo? Sheria inasema katikati ya wiki watu waanze kunywa saa 10:00 jioni na mwisho wa wiki saa nane, hebu shughulikieni nao wanaokwenda kinyume ili faini zitusaidie kwenye mambo mengine, kwa sababu hicho ndicho kisababishi kikuu cha mauaji yanayotokea Dodoma," aliagiza.

> **"Tabia hii katika mkoa huu imekuwa kikwazo katika kukabiliana na matukio ya ukatili ambayo asilimia 60 yanaanzia majumbani.**

Vilevile, alionya baadhi ya hospitali zinazotoza fedha wajawazito wanapokwenda kupata matibabu, akisisitiza huduma hiyo ni bure; atakayetozwa apige simu katika ofisi yake.

Pia alipongeza Mtandao wa Kijinsia Tanzania (TGNP) kwa kufikisha elimu ya ukatili wa kijinsia mkoani kwake huku akiwaomba kufanya hivyo katika wilaya nyingine.

Mkurugenzi wa TGNP, Lilian Lihundi, alisema mtandao huo utaendelea kutekeleza malengo ya Beijing kwa kushirikiana na mashirika yanayotetea haki za wanawake na usawa wa jinsia nchini.

Alisema pia wataendeleza vuguvugu la kushawishi wanawake kuwania nafasi za uongozi ili wajitambue na waondokane na manyanyaso.


Alisema lengo la kupeleka tamasha hilo Kondoa ni kutokana na takwimu kuonesha wilaya hiyo bado ina changamoto nyingi za ukatili wa kijinsia.

"Tunafahamu kwamba changamoto ya mimba za utotoni ni kubwa katika Wilaya ya Kondoa, lakini ni jambo linalohitaji juhudi kubwa kuanzia ngazi ya jamii na serikali hata leo tulivyokuwa na Mkuu wa Wilaya (Fatma Nyangasa), alisema anafanya tathmini ya kina ili aje na mikakati ya kukabiliana nazo.

"Ni matatizo ambayo kwa kiasi kikubwa yamejikita katika mila na desturi na yanahitaji nguvu za pamoja kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050 mimba za utotoni iwe historia," alisema Lilian.

Mshauri Mwelekezi katika Masuala ya Jinsia, Sanaa na Maendeleo, Agness Lukanga, alisema katika miaka 30 iliyopita tangu Mkutano wa Beijing, kuna uelewa mkubwa kuhusu masuala ya kijinsia ingawa matukio ya ukatili wa kijinsia yameongezeka na kasi ya kuripoti matukio hayo pia imeongezeka.

## KABWELA Na Fadhili Mohammed



# TRA Iringa yatenga siku maalum kusikiliza kero

**Na Agustino Kihombo**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Iringa imetenga Alhamisi kila wiki kuwa ni maalum itakayotumika kushughulika na upokeaji wa maoni, kero na ushauri kutoka kwa wananchi na wafanyabiashara.

Lengo ni kuboresha utoaji wa huduma na kuhamasisha wananchi kulipa kodi kwa hiari.

Akizungumza na Nipashe baada ya hafla ya uzinduzi wa siku ya kusikiliza walipakodi iliyofanyika Manispaa ya Iringa, Meneja wa TRA wa Mkoa, Aziz Rajab, alisema wameamua kuja na utaratibu huo kwa lengo la kuwasogeza karibu wafanyabiashara na mamlaka hiyo.

Alisema siku hiyo itatumika pia kutoa elimu ya kodi ili kuhamasisha ulipaji wa hiari na kuboresha mahusiano baina ya pande hizo mbili.

TRA imekuja na utaratibu huo ikiwa na lengo la kusogeza huduma kwa jamii, pamoja na kurahisisha usikilizaji wa kero za wafanyabiashara ambazo kwa namna moja au nyingine zimekuwa zikilalamikiwa na kukosa ufumbuzi jambo lililosababisha wafanyabiashara kushindwa kulipa kodi kwa wakati.

“Leo tumekuwa na zoezi la uzinduzi wa siku ya kusikiliza walipa kodi, siku hii ni muhimu sana kwetu sisi kama TRA kwasababu inatusogeza karibu na wananchi pamoja na wafanyabiashara kwa muda mrefu wamekuwa na malalamiko yao ya kodi na wameshindwa kupata majibu sasa tumeona ni vyema kutenga siku moja katika juma ambayo ni siku ya Alhamisi, hii itakuwa maalumu kwa ajili hiyo,” alisema Rajab.

Kuhusu hali ya ulipaji wa kodi, alisema katika Mkoa wa Iringa mwitikio umeendelea kuwa mzuri hii ni kutokana na elimu inayoendelea kutolewa na kuhamasisha kwa kiasi kikubwa wafanyabiashara kulipa kodi licha ya kuthibitisha baadhi ya zinawafanya kushindwa kuwajibika.

Akizundua siku hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Kheri James, alieleza serikali ilivyojipanga kuendelea kuboresha mazingira ya kibiashara na kufungua milango kwa wafanyabiashara kuwa huru katika shughuli zao ili waweze kulipa kodi bila bughudha jambo na kuwapo ukuaji wa uchumi kwa maendeleo ya taifa

Aidha, Mkuu huyo wa wilaya aliwataka TRA kuendelea kutumia nguvu katika utoaji wa elimu na kuwajengea uelewa wa manufaa ya kodi wananchi badala ya kutumia nguvu kuwakandamiza hali itakayosababisha biashara nyingi kufungwa.

“Serikali imedhamiria kuwawezesha wafanyabiashara kufanya biashara zao bila kubughudhiwa na mtu, na ndiyo maana kila kukicha inawaza namna gani bora itawawezesha kufanyabiashara kwa tija, lengo ni kukufanya uzalishe upate faida na uweze kulipa kodi, kwahiyo niwahakikishie tutaendelea kushirikiana katika kila hatua kwasababu mnapofanikiwa ndiyo mnaweza kulipa kodi kwa wepesi,” alisema James.

Aidha, alisema licha ya mamlaka hiyo kuweka mkazo katika suala la ukusanyaji wa kodi, suala hilo linapaswa kuwa rafiki bila kuathiri misingi ya biashara na badala yake ukusanyaji kodi uwe wenye kuwawezesha wafanyabiashara kuhamasika kulipa kodi.

Baadhi ya wafanyabiashara walioshiriki katika hafla hiyo walieleza namna siku ya kusikiliza walipakodi itakavyosaidia kuimarisha uhusiano baina yao huku wakiikumbusha TRA kuendelea kuwajengea uwezo wafanyabiashara badala ya kuwarudisha nyuma hususani katika biashara.

# Wawakilishi Zanzibar wapongeza NSSF kiutendaji

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, chini ya Mwenyekiti, Mwanaasha Khamis Juma, wameupongeza Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yake ya msingi ambayo ni kuandikisha wanachama, kukusanya michango, kuwekeza na kulipa mafao.

Mwanaasha ametoa pongezi hizo wakati walipofanya ziara ya kikazi NSSF jijini Dar es Salaam, kwa lengo la kujifunza utendaji kazi wa Mfuko ikiwamo matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma na hatua mbalimbali ambazo ilipitia toka ulipoanzishwa mpaka sasa.

“Sisi kama Kamati ya Bajeti tunawashukuru sana NSSF na tumefaidika kwa namna moja ama nyingine, tumeona kwa upande wa uwekezaji tunawapongeza kwa kufikia hatua kubwa ya uwekezaji pamoja na matumizi ya TEHAMA,” alisema Mwanaasha.

Alisema NSSF imepiga hatua kubwa kiutendaji ikiwamo kufanya maboresho mbalimbali kama mifumo ya fedha, mifumo ya uandikishaji, ukusanyaji michango na ulipaji wa mafao.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Soud Nahodha Hassan, alipongeza utaratibu ambao NSSF inafanya hususan kwenye utekelezaji wa majukumu yake ya msingi jambo ambalo limechochea mafanikio.

Mjumbe wa kamati hiyo, Asha Abdallah Juma, alisema amefurahishwa na kazi kubwa zinazofanywa na NSSF hasa katika ukusanyaji wa michango ya wanachama toka ilipoanzishwa mpaka sasa.

Suleiman Masoud Makame amepongeza mabadiliko mbalimbali yaliyofanywa na NSSF toka ikiitwa NPF mpaka sasa na imepiga hatua kubwa ya kiutendaji.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, alisema Mfuko umeboresha huduma zake kupitia mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kurahisisha huduma kwa wanachama ili waweze kuzipata hukohuko waliko bila ya kulazimika kufika ofisi za NSSF.

Mshomba alisema maeneo mengine ambayo wameyaboresha ni ukaguzi, uwekezaji na utendaji kwa ujumla jambo ambalo limechagiza mafanikio na kwa sasa thamani ya Mfuko imefikia trilioni 8.6.

PATHFINDER

## PATHFINDER INTERNATIONAL

This Publication is made in accordance with regulation 13 (a) of the Non-Governmental Organizations (Amendments) Regulations ,2018 which obliges Non-Governmental Originations receiving funds exceeding twenty million shillings to publish funds received and its expenditure in a widely circulated newspapers and other media channels which are easily accessible by the target beneficiaries.

**EXPENDITURE INCURRED IN THE PERIOD OF JAN-JUNE 2024**
**Figure are in TZS in '000**

| Cost categories | MC-IMA/USAID-MOMENTUM 1 | [TZ2302] TZ-JGI-Hope Through Action Activity | TZ-EngenderHealth-DFID FP Scale Up | TZ-UNICEF-Provider Bias Expansion | TZ-Bergstrom-MYKY | TZ-OakFoundation-Kuwaza Phase 3 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Personnel | 367,776 | 358,526 | 410,908 | 58,484 | 108,625 | 141,171 |
| Consultants | 0 | 0 | 0 | 88,035 | 0 | 13,655 |
| Professional Services | 3,399 | 0 | 115 | 307 | 1,014 | 2,172 |
| Travel and Transportation | 119,982 | 55,837 | 87,627 | 33,010 | 33,610 | 20,789 |
| Occupancy | 63,438 | 33,114 | 36,913 | 2,945 | 19,097 | 30,465 |
| Supplies and Equipment | 36,917 | 34,118 | 0 | 0 | 31,766 | 11,511 |
| Staff Development | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Participant Training | 299,078 | 339,066 | 2,424 | 34,852 | 74,651 | 38,611 |
| Other Office Costs | 11,195 | 10,435 | 7,298 | 803 | 2,936 | 2,061 |
| Subawards | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 160,443 |
| Depreciation | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Non-Operating | 2,590 | 2,570 | 65,242 | 741 | 820 | 838 |
| **Total Expense** | **904,375** | **833,666** | **610,527** | **219,177** | **272,520** | **421,718** |

| Cost categories | TZ-JohnSwift-TZ Swift PHE | TZ-Cargill-Integration & Sustainability Tuungane | TZ-Vodafone-M-MAMA 3 | TZ-Anonymous-CGD Advancing Abortion Rights IX | TZ-Bergstrom-CPAC Expansion | Pathfinder Global |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Personnel | 44,157 | 187,509 | 1,425,832 | 82,889 | 113,231 | 175,684 |
| Consultants | 1,219 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Professional Services | 0 | 0 | 2,514 | 150 | 575 | 16,072 |
| Travel and Transportation | 2,323 | 11,622 | 317,097 | 14,743 | 46,932 | 19,284 |
| Occupancy | 5,085 | 36,020 | 299,091 | 26,327 | 18,144 | -239,820 |
| Supplies and Equipment | 0 | 26,586 | 67,226 | 10,112 | 1,936 | 96,436 |
| Staff Development | 0 | 0 | 620 | 0 | 0 | 2,383 |
| Participant Training | 0 | 62,416 | 1,914,362 | 57,470 | 44,280 | -248 |
| Other Office Costs | 66 | 26,800 | 100,946 | 2,696 | 1,464 | 179,401 |
| Subawards | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Depreciation | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1,813 |
| Non-Operating | 134 | 779 | 11,642 | 541 | 587 | 643 |
| **Total Expense** | **52,983** | **351,732** | **4,139,332** | **194,929** | **227,147** | **251,650** |



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo (katikati), akifanya ziara ya kuangalia mradi wa kimkakati wa magadi soda Engaruka, wilayani Monduli, mkoani Arusha jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), Dk. Nicolaus Shombe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watakaopisha ujenzi kiwanda magadi soda kulipwa mabilioni

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 14 kwa ajili ya kuwalipa fidia wakazi wa Kata ya Engaruka, Wilaya ya Monduli mkoani hapa kupisha ujenzi wa kiwanda cha magadi soda.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Viwanda na Biashara, Seleman Jafo, alipotembelea mradi wa kimkakati wa magadi soda hayo uliopo katika kata hiyo unaotekelezwa na Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC).

Jafo aliwahakikishia wakazi hao kuwa, kila anayestahili kulipwa fidia atapewa haki yake na kuwataka kuacha kujihusisha na vitendo vya udanganyifu kwa kuwa serikali ilifanya uhakiki wa majina ya wanaostahili.

Aliutaka uongozi wa Wilaya ya Monduli, kupima maeneo yanayozunguka mradi huo kwa ajili ya ujenzi wa makazi, viwanda na biashara kwa mpangilio unaovutia.

Alisema serikali itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na umeme ili kurahisisha utekelezaji wa mradi huo; ubebaji, ufungaji wa mitambo ya kiwanda hicho.

Jafo, alisema madini hayo ni muhimu kwa kuwa yatasaidia viwanda vya uzalishaji wa vioo, dawa na bidhaa zitakazouzwa ndani na nje ya nchi.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Festus Kiswaga, alisema wameupokea mradi huo na kutoa rai kwa wananchi kuchangamkia fursa zitakazotokana na utekelezwaji wake.

Mkurugenzi Mtendaji wa NDC, Dk. Nicolaus Shombe, alisema wao kama mwekezaji kwa niaba ya serikali, wamekamilisha hatua za awali kuelekea kuanza utekelezaji wa mradi huo. Dk. Shombe, alitaja baadhi ya hatua hizo kuwa ni kufanya tafiti za ubora wa magadi, upembuzi yakinifu, tathmini ya athari kwa mazingira, mali za wananchi na usanifu wa ujenzi wa kiwanda hicho.

Alisema ujenzi wa kiwanda hicho utakapokamilika, kitakuwa na uwezo wa kuzalisha magadi tani milion moja za magadi soda kwa mwaka.

Takwimu zinaonesha kuwa, Monduli ina mita za ujazo trilioni 4.7 za magadi soda katika vijiji vya Engaruka na Selela.

## Wachimbaji tanzanite waagizwa kuisaidia jamii

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

UONGOZI wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani wilayani hapa Mkoa wa Manyara, umewaagiza wawekezaji na wachimbaji wa madini ya Tanzanite kuisaidia jamii inayowazunguka.

Agizo hilo limetolewa na Ofisa Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Isack Mgaya wakati Mkurugenzi wa Kampuni ya Heroes Mining Camp, Basil Njau, akikabidhi msaada wa vyakula kwa watoto yatima.

Mgaya alifafanua kuwa, agizo hilo ni kwa mujibu wa sheria inayowataka wawekezaji na wachimbaji hao kuisaidia jamii inayowazunguka kwa kutoa kiasi cha pato kutokana na shughuli za uchimbaji.

Alisema sheria inawataka wachimbaji kufanya hivyo kwa kuwa shughuli za uchimbaji zinapofanyika zinakuwa zimewanyima fursa baadhi ya wenyeji hivyo wanapaswa kuangaliwa kwa jicho la tatu kwa kutoa misaada.

"Tunaipongeza Kampuni ya Heroes Mining Camp kupitia Mkurugenzi wake, Basil Njau kwa kuwa bado hawajaanza uzalishaji, lakini wametoa shilingi milioni mbili kusaidia watoto yatima," alisema.

Mwenyekiti wa Shirika lisilo la kiserikali la Saidia Wanajamii Tanzania (SAWATA), liliondaa na kuratibu shughuli hiyo, Mohamed Mughanja, alitumia fursa hiyo kumshukuru mkurugenzi wa kampuni hiyo kwa kutoa msaada kwa wahitaji hao.


MANYARA SUGAR COMPANY LIMITED

TAARIFA KWA UMMA

KAMPUNI YA SUKARI YA MANYARA SUGAR INAPENDA KUUTAARIFU UMMA YA KWAMBA BIDHAA ZAKE ZINAPATIKANA KWA WAKALA HAWA WAFUATAO:

| S.NO | JINA LA WAKALA | MAHALI | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|
| 1 | ARUSHA SUNDRIES LTD | ARUSHA | 0689324772 |
| 2 | SAMWELI KASTULI | KARATU | 0754761198 |
| 3 | PETER MALLYA | BABATI | 0784689785 |
| 4 | D.D.GENERATION&CO | BABATI | 0788535076 |
| 5 | GODFREY PASCHAL | BABATI | 0756677484 |
| 6 | ROBERT OLOMI | BABATI | 0784396064 |
| 7 | PRISCUS MUSHI | BABATI | 0655112800 |
| 8 | NADE SHOP | BABATI | 0789969689 |
| 9 | EVANS MACHA | BABATI | 0782460083 |
| 10 | FESTO ELIAS MUSHI | BABATI | 0683702442 |
| 11 | NANCY ALEX LAUWO | BABATI | 0784758607 |
| 12 | AGUSTINO HAMNAI | KATESH | 0787374125 |
| 13 | JOSEPHINA DANIEL | KATESH | 0784419509 |
| 14 | JULIAS CHRISTOPHER | KATESH | 0786687007 |
| 15 | R.K. TAYAL | MAGUGU | 0786268085 |
| 16 | MARTIN AKONAY | MATUFA | 0787656687 |
| 17 | DAUDI SHAURI | MAGARA | 0682489575 |
| 18 | ATHUMANI SIMBIRE | LOLIONDO | 0672 413636 |
| 19 | LAWI ALI AKONAY | LOLIONDO | 0788367062 |
| 20 | ALEX MICHEL | ENDASAK | 0683228090 |
| 21 | AWAZ HAJI | ENDASAK | 0782929480 |
| 22 | JAFARI RAJABU GUKA | KITETO | 0788089061 |
| 23 | MOHAMED A.KIJU | KONDOA/CHEMBA | 0784920350 |
| 24 | SALUM SEIF SALUM (AFISA MASOKO) | NZEGA/KAHAMA/TABORA | 0754388954 |

KWA MAWASILIANO ZAIDI TAFADHALI PIGA NAMBA HII YA SIMU IFUATAYO:

UTAWALA
MANYARA SUGAR COMPANY LIMITED
S.L.P.3122 ARUSHA
baruapepe:info@manyarsugar.co.tz, simu :0622070700



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA MARA, SIMIYU NA MANYARA (BABATI DC, HANANG DC, MBULU DC NA BABATI TC)

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza na mzunguko wa nne utafanyika katika Mikoa ya Mara, Simiyu, na Manyara katika Halmashauri za Wilaya za Babati, Hanang, Mbulu na Mji wa Babati tarehe 04 hadi 10 Septemba, 2024. Zoezi la uboreshaji wa Daftari litafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Jumatano tarehe 04 hadi Jumanne tarehe 10 Septemba, 2024.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume ***www.inec.go.tz*** au anuani ya ***ovrs.inec.go.tz*** kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 9 na kubonyeza.Kisha atachagua Namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

***KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***
**Limetolewa tarehe 27 Agosti, 2024 na:**

Juma Rahisi,
KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI





# Wanafunzi wadaiwa kuacha shule kwa kuhofia kutekwa

**Na Vitus Audax,** TABORA

WAKAZI wa Kijiji cha Ng'ere Kata ya Mwasala Wilaya ya Nzega mkoani hapa wamedai baadhi ya watoto wao wameacha shule kwa kuhofia kutekwa na kuchunwa ngozi na watu wasiojulikana.

Walitoa madai juzi kwa maofisa wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) walipofanya ukaguzi wa vituo vya Polisi na Magereza wilayani humo na Igunga na kusikiliza kero za wananchi.

Mkazi wa Kata ya Mwasala, Angelina Dotto, alisema hali ya matukio yanayoendelea kutajwa kutokea mara kwa mara katika mkoa huo na mikoa jirani imeleta taharuki na kuongeza woga kwa watoto wao.

"Kinachoendelea kwa sasa ni kuwalazimisha kwenda shule lakini ukiwalazimisha zaidi wanaacha masomo yao na pengine kujinyonga wakidai wanapokuwa njiani kuelekea shule iliyopo umbali mrefu wanachunwa ngozi," alisema Angelina na kuongeza kuwa;

"Kwa kuwa na sisi ni wazazi inatubidi tuwasubirishe hadi kukuche ndiyo waende shule, lakini bado wakichelewa huko shule wanaadhibiwa bila kujali hali wanazopitia wakirudi nyumbani hawatamani kabisa kuendelea na masomo."

> **"Kinachoendelea kwa sasa ni kuwalazimisha kwenda shule lakini ukiwalazimisha zaidi wanaacha masomo yao na pengine kujinyonga wakidai wanapokuwa njiani kuelekea shule...**

Mkazi mwingine, Malonda Maganga, alisema wanafunzi wanatoka Busanda kwenda kusoma Ngelengele hata wadamke vipi ni lazima wachelewe na kuiomba serikali kusogeza huduma hiyo karibu.

Ofisa Tarafa wa Puge, Moses Ndondoye, alisema ili kutatua kero za wananchi ipo haja ya ofisi za tume hiyo kusogezwa ngazi ya wilaya na kudhibiti uhalifu na utekaji wa watoto.

Makamu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Mohammed Hamis Hamad, aliahidi kufuatilia madai ya utekaji wa watoto na kufanya uchunguzi ili kubaini waliko baadhi.

Alivitaka vyombo vya dola kutoa taarifa haraka juu ya hatua wanazozichukua kufuatia matukio hayo ili kuepusha taharuki kwa wananchi na kusababisha maandamano yasiyo ya lazima kushinikiza polisi kutoa taarifa kama ilivyotokea mkoani Simiyu.



Daktari wa Kinywa na Meno kutoka Hospitali ya Kanda ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi (JWTZ) Mwanza, Meja Simon Mushi, akimhudumia mgonjwa hospitalini hapo juzi, ikiwa ni mwendelezo wa huduma za uchunguzi, vipimo na matibabu bure kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya jeshi hilo, ambapo huduma hizo pia zinatolewa katika viwanja vya Furahisha, jijini humo. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Vijana wahadharishwa 'madada poa'

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

VIJANA katika Kijiji cha Masengwa wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga, wametakiwa kujiepusha na wanawake kutoka mjini wanaofika kwenye maeneo yao kwa lengo la kujiuza kipindi cha mavuno ili kujikinga na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi na Ukimwi (VVU).

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Sambo Sanane, wakati akizungumza na Nipashe kijijini hapo kufuatia ongezeko la wanawake hao maarufu kama dada poa kutoka mjini hasa wakati wa mavuno.

Alisema kipindi cha mauzo, madada hao wengi wa mjini wanamiminika vijijini kwa ajili ya kufanya biashara ya kwa kupewa pesa au mazao hali inayosababisha ongezeko la maambukizi hayo na kuziacha familia na umaskini baada ya mazao kwisha. Alisema wameweka nguvu kubwa kuwaelimisha, vijana athari za biashara hiyo ya ngono na kujikinga na maambukizi ya virusi hivyo.

Mtendaji wa Kijiji cha Masengwa, Paschal Chubwa, alisema wamekuwa wakipiga marufuku wasichana wadogo kujihusisha na mapenzi ili kutimiza ndoto zao. Baadhi ya wazee wa mila kijijini humo, akiwamo Yasunga Kitindi, alisema vikao vya familia 'Shikome' vinapaswa kurudishwa ili wazazi wazungumze na vijana wao na kuwapatia elimu ya stadi za maisha. Alisema vijana wengi wamekuwa na mmomonyoko wa maadili kutokana na wazazi wao kushinda kwenye vijiwe vya kahawa kupiga porojo huku wakisahau kuwafunda watoto wao.

## Serikali yaamuru mkandarasi kurejea nchini kujieleza

**Na Vitus Audax**

SERIKALI imempa siku 14 mkandarasi wa Kampuni ya Ujenzi ya Sichuan Road na End Bridge Ground Corporation Ltd ya nchini China, kurejea nchini kujieleza kwa kushinda kukamilika kwa mradi wa barabara ya Tactics mkoani Geita.

Mkandarasi huyo licha ya kudaiwa kulipwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 17 kwa wakati, anadaiwa kusababisha kero kwa

wananchi kwa kushindwa kusafiri na kusafirisha mazao yao.

Agizo hilo dhidi ya mkandarasi huyo, lilitolewa juzi wakati Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Miundombinu wa Wizara ya Ujenzi, Rogatus Mativila, alipotembelea mradi huo na kubaini kuwa upo nyuma kwa utekelezaji.

"Mradi huu ulikuwa utekelezwa ndani ya miezi 15 na ulitakiwa ukamilike mwezi wa pili mwakani na kwa sasa imebaki miezi sita tu kazi iliyofanyika haionekani," alisema Mativila.

Mkurugenzi wa Tactics nchini, Lucas Nyaki, alisema serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 22 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo zenye urefu wa zaidi ya kilomita 17.

"Tatizo katika mradi huu ni mkandarasi alitakiwa vitendea kazi alivyonavyo kuwa eneo la kazi kwa asilimia 100, lakini ana asilimia 53 hali inayosababisha kuchelewesha kazi," alisema Nyaki.

Baadhi ya wakazi wa Geita, akiwamo Amina Athumani waliomba serikali kusimamia ipasavyo ujenzi wa barabara ili kuhakikisha zinakamilika na kumaliza adha ya usafiri na usafirishaji wa mazao.

## TCB yataka kilimo chenye tija

**Na Halima Ikunji,** TABORA

OFISA Kilimo Mkuu wa Bodi ya Pamba Tanzania (TCB) Kanda ya Magharibi, Bluma Kalidushi, amewataka wakulima wa pamba nchini kuendesha kilimo chenye tija kwa kufuata kanuni, taratibu na maelekezo ya wataalamu wakati wa kuandaa mashamba hadi mavuno.

Alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa.

Alisema kilimo chenye tija kina manufaa makubwa kwa wakulima kwa kuwa kinaongeza uzalishaji na kumwezesha mkulima kupata mazao bora.

Alibainisha kuwa baadhi ya wakulima wamekuwa hawazingatii maelekezo ya wataalamu kuanzia mwanzo na wakati wa mavuno hali inayopelekea baadhi yao kuweka takataka.

ALHAMISI AGOSTI 29, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

**Mafuta ya kokwa, mbegu matunda yana utajiri afya lishe kupindukia**



Ukurasa 14

**Hospitali Bombo; sasa mkombozi wa watoto 'njiti', kituo tiba viungo**

MAZINGIRA

RAIS NA AJENDA KUMTUA MAMA NDOO...

# Mwenge Uhuru wakagua kilichoagizwa RUWASA, kunakolengwa 'maji bombani'

• Shinyanga: 15,500 watumia maji Victoria; subira vijiji 97

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MTU anapotaja msamiati 'maji' una tafsiri pana, kwamba ni kitu chenye mustakabali mpana sana katika maisha ya umma na viumbe hai vingine.

Ni hatua maji yanabaki na tafsiri ya maendeleo ya kijamii, hadi kiuchumi, huku mwongozo wa Sera ya Maji ya Mwaka 2002 nchini, inasema wananchi wa vijijini wanapaswa kupata huduma ya maji kwa asilimia 85 huku mijini ikibaki asilimia 95.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, naye akiweka katika ajenda zake kuu ya malengo kitaifa, katika tafsiri ya kumletea unafuu Mtanzania na hususan mwanamke aliyeko kijijini akifuata maji umbali mrefu, ameibebesha msamiati ni 'Ajenda ya kutua ndoo.'

Katika sura ya utekelezaji kuanzia mzizi wa sera tajwa, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa), ilianzishwa mwaka 2019 na tangu hapo imekuwa inatekeleza miradi ya maji vijijini, lengo mojawapo 'kumtua ndoo kichwani mwanamke, kumwondolea adha ya kufuata maji umbali mrefu."

Mnamo Agosti 10 mwaka, mbio za Mwenge wa Uhuru zikiwa mkoani Shinyanga, zikazindua miradi mitano ya maji safi na salama katika halmashauri tano za mkoa; Kishapu,Wilaya ya Shinyanga, Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama, zinazotekelezwa na Ruwasa.

Meneja wake wilayani Kishapu, Mhandisi Dicksoni Kamazima, anasema mradi ambao umezinduliwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru ukiwa Seseko hadi Ngundangali, kwa maji kutoka Ziwa Victoria, ukinufaisha wananchi 15,500, akifafanua: "Mradi huu wa maji, chanzo chake ni Ziwa Victoria na gharama zake ni shilingi bilioni 2.8."

Meneja wa Ruwasa wilayani Kahama, Mhandisi Maduhu Magili, anasema katika eneo lake, miradi mitatu ya maji imezinduliwa na Mwenge wa Uhuru, ikiwanufaisha wananchi 2,400 kwa gharama shilingi milioni 64.6 na upanuzi wake hadi kwa wanavijiji 9,268 wa Manispaa ya Kahama; pia katika Halmashauri ya Ushetu, utanufaisha wananchi 7,563 katika vijiji viwili.

"Wananchi wa vijiji hivi hawakuwa na maji kabisa, lakini Ruwasa tukaona tutoe kipaumbele," anasema Mhandisi Magili.



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024, Godfrey Mnzava, alipozindua mradi wa majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria katika vijiji vya Seseko na Ngundangali, wilayani Kishapu, na kuwanufaisha wakazi 15,500 mwezi huu. **PICHA: MARCO MADUHU**

**KIKOHOZI CHA WABUNGE**

Mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo, anasimulia mateso ya muda mrefu ya wananchi wake waliokosa maji safi na salama, sasa kukishuhudiwa mageuzi kuwapo huduma ya majisafi na salama.

Huku akidokeza yamebakia maeneo machache kufikiwa na huduma rasmi za maji, Butondo anaeleza: "Wilaya ya Kishapu ni kame sana! Kipindi cha kiangazi, wananchi walikuwa wakipata shida ya kupata maji na hata kuchangia maji na mifugo..."

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, anasema wananchi wa jimbo lake bado wako katika hali mbaya ya ukosefu wa maji safi na salama, akiomba Ruwasa iongeze juhudi za usambazaji mtandao wa maji, ili kuvifikia vijiji, kufanikisha "kumtua ndoo kichwani mwanamke.'

Naye, Mbunge wa Solwa, Ahmed Salum, anasema katika vijiji 126 vilivyopo wilayani Shinyanga, matarajio yaliyoko kwamba hadi kufikia mwakani 2025 vyote vitakuwa na maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria.

Anasema hadi mwaka huu 2024, vijiji ambavyo havijafikiwa na huduma ya maji safi na salama, viko 97 na tayari viko kwenye mchakato wa kupelekewa huduma hiyo.

**WAKIMBIZA MWENGE**

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024 Godfrey Mnzava, anasema katika utekelezaji miradi hiyo ya maji, wananchi wanapaswa ku-

Inaendelea Uk. 12

AFYA

# Polisi Dar wajitosa mtaani vita ukatili unaoendelea kwa watoto

**Na Sabato Kasika**

MATUKIO ya ukatili wa kijinsia, ni miongoni mwa yale yaliyoshamiri ndani ya jamii yakiumiza makundi mbalimbali, wakiwamo watoto wadogo.

Kutokana na mazingira hayo hatarishi, Jeshi la

Polisi Mkoa wa Kipolisi wa Ilala Dar es Salaam, limeamua kuanzisha kampeni ya miezi sita ya kuwaepusha na vitendo hivyo, vikiwamo ulawiti na ubakaji.

Ni kampeni iliyopewa jina 'Tuwaambie Kabla Hawajaharibiwa', iliyoanza wiki iliyopita na inatarajiwa kuhitimishwa Februari mwaka ujao.

Mbali na shule za msingi, sekondari na vyuo, kampeni hiyo itafikishwa katika nyumba za ibada, pia kwenye vijiwe mbalimbali, vikiwamo vya bodaboda.

Mratibu wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa utendaji kazi askari wa madawati ya jinsia na watoto mkoa huo wa kipolisi, Inspekta wa Polisi, Dk. Christina Onyango, ndiye anayesema wakati wa kufunga mafunzo hayo mjini Dar es Salaam, wiki iliyopita.

Anasema, matukio mengi yanayoripotiwa katika vituo vya mkoa huo ni ya ulawiti na ubakaji na kwamba, wameona waanzishe kampeni ya kutoa elimu itakayosaidia kuepuaha makundi hayo na ukatili huo, ili kunusuru kizazi kijacho.

"Tutatoa elimu kwa wanafunzi wa shule za msingi na wote wa vyuo, lakini wa sekondari ni kwa kidato cha tano na sita," anasema.



Polisi wakiwa katika mafunzo, kabla ya kutawanywa kufanya kampeni ya kupambana na ukatili wa kijinsia kwa watoto, wilayani Ilala. **PICHA: SABATO KASIKA**

**JINSI ITAKAVYOKUWA**

Afande Dk. Christina anasema, wakuu wa madawati ya jinsi na watoto, watakuwa wanazuru katika shule za msingi, sekondari na vyuo, wakiitisha midahalo na kujadili madhara ya vitendo, wakiwapa nafasi wanafunzi kujieleza.

"Kwa mfano, wale wa shule za msingi tunataka kuwaelimisha madhara ya ukatili wa kijinsia ikiwamo rushwa ya ngano pia," anasema.

> **"Wazazi na walezi hawana muda wa kusimamia malezi bora, wako 'bize' na mambo yao, watoto wamejiingiza katika mambo yasiyofaa, kwa sababu ya kukosa malezi.**

Anafafanuwa kuwa, wahusika hao watafundishwa pia kutambua viashiria vya ukatili wa kijinsia na namna ya kutoa taarifa, ili watuhumiwa wakamatwe na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

"Katika 'vijiwe', sehemu za biashara na nyumba za ibada, tutawaelekeza wazazi na walezi kuzingatia umuhimu wa malezi bora ili watoto waendelee kuwa salama," anasema.

Dk. Christina anasema, baadhi ya wazazi na walezi hadi sasa wamekuwa wanazembea, wakiwaacha watoto wanajilea wenyewe, huku ndugu wa karibu wakihusika katika vitendo hivyo. Kwa hiyo tunataka wajue umuhimu wa malezi bora," anasema.

Anafafanua kuwa mmomonyoko wa maadili ni tatizo kwa nchi nzima, akiamini katika eneo lake askari wenzao wa mikoa mingine wako kwenye mikakati ya kufanya kampeni kama hiyo.

**ANGALIZO KWA POLISI**

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto Mkoa wa Kipolisi wa Ilala. ASP Gloria Urassa, anatoa angalizo kwa polisi wa dawati hilo watakaoenda kufanya kampeni hiyo, wazingatie maadili kwa kufuata kaulimbiu ya jeshi hilo anayoitaja kuwa ni nidhamu, haki na weledi.

"Ili askari aonekane ana nidhamu, tunazingatia mambo kadhaa kama uvaaji wake, kuwahi kwenye tukio, kutoleta taharuki kwenye jamii, kwani tumekuwa tukifanya kazi kwa watu walioumizwa kimwili na kisaikolojia," anasema ASP Glory.

Anasema, askari hapaswi kuchanganya mambo yake ya nyumbani anapokuwa anashughulikia sera za madawati ya jinsia au kutanguliza urafiki ama upendeleo, bali azingatie haki, nidhamu na weledi.

"Huko mnakokwenda kufanya kampeni, mtaletewa waathirika wa ukatili wa kijinsia, hivyo, ni muhimu mtumie weledi wenu vizuri mnapojadiliana nao. Lugha nzuri kutoka kwa askari wa dawati la jinsia ni ya muhimu." anasema.

Aidha, anasema mkoa huo una wilaya za kipolisi tano za Buguruni, Kariakoo, Chanika, Ukonga na Kati zikiwa na madawati tisa ya jinsia na watoto.

Mratibu wa Diwani la Usalama Wetu Kwanza, wilaya ya Kipolisi ya Kariakoo na Kati Mkaguzi wa Jeshi la Polisi, Japhet Shilla, anasema malezi duni na teknolojia ni chanzo cha mmomonyoko wa maadili katika jamii.

"Wazazi na walezi hawana muda wa kusimamia malezi bora, wako 'bize' na mambo yao, watoto wamejiingiza katika mambo yasiyofaa, kwa sababu ya kukosa malezi.

"Hivyo, tunakwenda kuwakumbusha kila mmoja atimize wajibu wake ili kupunguza tatizo la ukatili wa kijinsia," anasema Shilla.

Inspekta wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lydia Mrema, anasema wazazi na walezi watenge muda wa kukaa na watoto wao, pia wajenge urafiki nao ili hata watoto wanapokuwa na matatizo, wawe huru kuwaambia.

"Watoto Wana vitu vingi wanavyokumbana navyo shuleni, mitaani na hata nyumbani, lakini hawawezi kuvisema kama wazazi na walezi hawako karibu nao," anasema Lydia.

Mkuu wa Kituo cha Polisi Kati, ASP Sophia Dilunga, anasema bila wazazi wa kike kubadilika na kusimamia malezi ya watoto, vita dhidi ya ukatili wa kijinsia inaweza kuchukua miaka mingi.

"Ninasema hivyo, kwa sababu sisi wanawake ndio tunaokaa na watoto kwa muda mrefu, lakini bahati mbaya hatusimamii malezi kikamilifu, tuwakumbushe hilo tunapokwenda kutoa elimu," anasema ASP Sophia.

# Mwenge Uhuru wakagua kilichoagizwa RUWASA, kunakolengwa 'maji bombani'

**Inatoka Uk. 11**

vutiwa maji majumbani mwao, ili kutekeleza dhana ya Rais Dk. Samia ya 'kumtua ndoo kichwani mwanamke, kwa kuchota maji bombani nyumbani kwake na siyo kwenye vituo.'

Anasema Rais Samia amekuwa akiidhinisha fedha za miradi ya maji ili kumtua ndoo kichwani mwanamke na akaitaka Ruwasa iongeze kasi ya kusambaza huduma ya maji kwa wananchi katika maeneo mengi vijijini.

"Huduma ya maji haina mbadala, na kama kauli yenu ya Ruwasa inavyosema "Ruwasa maji bombani" endeleeni kusambaza maji zaidi kwa wananchi, na pia kuwaunganishia majumbani mwao ili kumtua ndoo kichwani mwanamke," anasema Mnzava.

Anawasihi pia wananchi ambao wametekelezewa miradi hiyo ya maji kwamba waitunze miundombinu yake na kutoifanyia hujuma, ili waendelee kupata kuhuma ya majisafi na salama kwa muda mrefu.

**WANUFAIKA WALONGA**

Mwanamke Sabina Lukas mkazi wa kijiji cha Chona Halmashauri ya Ushetu, anasema upataji wa majisafi na salama kijijini humo umewaondolea matatizo ambayo wamekuwa wakikumbana nayo, kwamba licha ya kuteseka kubeba ndoo kutoka umbali mrefu zaidi hata kilomita tatu pia ndoa zao zilikuwa mashakani wakisingizwa 'kuchepuka.'

Anasema ukosefu wa maji maeneo ya vijijini, wanaoteseka ni wanawake, kwa sababu ndiyo wanaolea familia, kuhakikisha anachokitafsiri "familia imekula na baba ameoga."

Pia, anasema inapokuwa wakichelewa kurudi kutoka safari ya kuchota maji, nako wanaulizwa maswali mengi hata kuishia ugomvi.

"Upatikanaji wa maji vijijini ni furaha kubwa sana kwetu sisi wanawake kwa sababu hata ndoa zetu zinakuwa na amani sana, licha ya kuteseka kubeba ndoo ya maji kichwani umbali mrefu,"anasema Sabina.

AFYA

MTAALAM NZALAWAHE TWAHIR:

# Mafuta ya kokwa, mbegu matunda yana utajiri afya lishe kupindukia

## • Tiba UTI, CD4, ngozi, vipodozi...

Na Pilly Kigome

KITAALAMU inatajwa matumizi ya mafuta ya mbegu na kokwa za matunda yanaleta mabadiliko kwenye mwili wa binadamu kwa kuimarisha afya na inatibu, pasipo kutegemea dawa za kisasa za kitatibu.

Kuna utafiti mbalimbali uliofanywa na wataalamu wa afya na lishe, unaotoa majibu chanya, huku katika Chuo Kikuu cha Afya na Tiba Muhimbili (MUHAS) kukiwapo kitengo kinachojikita katika eneo hilo, kutegemea nyenzo hizo asilia.

Nipashe ilimtafuta mtaalamu wa stadi hizo, anayejihusisha na uzalishaji, pia uuzaji wa mafuta ya mbegu na kokwa za matunda kwa matumizi ya binadamu, kupata ufafanuzi wake.

Huyo ni Nzallawahe Twahir, mwenye shamba na kiwanda kilichoko mkoani Iringa vinavyoongezea thamani bidhaa hizo, akitetea kitaalamu faida nyingi zitokanazo na mafuta hayo.

Twahir, ambaye ni Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao Mstaafu katika Wizara ya Kilimo, sasa anaisimamia kampuni yake, anaiambia Nipashe kwamba mwanadamu anayetumia mafuta yatokanayo na matunda, kwa mapishi na vipodozi ananufaika zaidi kiafya.

Anataja manufaa yaliyoko kwenye mafuta ya matunda na mbegu ni makubwa na bora zaidi, kuliko mafuta yaliyozoeleka kwa wengi katika matumizi ya kila siku.

Anafafanua, awali alijihusisha na biashara ya matunda pekee, ikamkatisha tamaa kutokana na faida ndogo, ndio baadaye akahamia mauzo ya matunda.

Mtaalamu huyo, anasimulia baadaye akapenya aliko sasa akianza na kufanya utafiti uliompatia elimu kuhusiana na faida zinazopatikana na tunda au kokwa za matunda, akaona afanye biashara ya kusaidia kuboresha afya za Watanzania, kwa kujihusisha na kutengeneza bidhaa za mafuta yatokanayo na matunda hayo.

Anaisimulia Nipashe kwamba, hiyo ilikuwa mwaka 2012 kwamba mbali na kuwa ekari 30 shamba la parachichi, wakati huo soko halikuwa zuri kama, akawa anajikita na kutoa faida yatokanayo na matunda anayoyafanyua kazi, akizalisha mafuta yanayouzwa ndani na nje ya nchi, ikileta tija katika afya za binadamu.

**MBEGU ZA MABOGA**

Twahir anaeleza kwamba matumizi ya mafuta anafananisha kuwa sawa na ubora wa mtu anayetumia samaki wa kawaida au dagaa, kutokana na kuwa na wingi wa viinilishe 'magnesium' na 'zinki'.



Twahir Nzallawahe, alipokuwa katika ziara ya kikazi katika zama akiwa Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi, katika Maonesho ya Nanenane Viwanja vya Ngongo, mkoani Lindi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Hapo anaitambulisha kuwa mbegu pekee inayotoa madini mengi, ambayo wataalamu wengi wa afya na lishe wanashauri wajawazito wayatumie kwa nafasi ya viungo katika chakula, ikizuia watoto kuzaliwa na hali ya mtindio.

Anafafanua kuwa, mjamzito anapotumia mafuta haya kila siku au unga utokanao na mbegu za maboga kwa, humsaidia kumkinga mtoto aliye tumboni na shida hiyo ya utindio.

Mtaalamu huyo anataja nafasi nyingine, ni kwamba inawasaidia watu wanaokosa usingizi, wenye mawazo (stress), pia inawawezesha wazee kupata usingizi kwa usahihi.

Lingine analieleza kwamba, watumiaji wanaongezewa 'Vitamin A' na viini vingi ukitofautisha, akiwa anafafanisha kwa ziada dhidi ya viinilishe kutoka mafuta ya kawaida ya kupikia.

Twahir anataja sifa nyingine zilizopo kwenye mafuta hayo, ni kwamba hayagandi hata yanapowekwa kwenye jokofu (friji).

Katika sura ya kijinsia, Twahir anawataja wanaume wanaotumia mafuta ya maboga au mbegu, inawafanya kuzuia tezi kutovimba, kwa sababu ya uwapo zinki kwenye mbegu hizo za maboga.

Hiyo inatajwa kuendana na kuzuia uvimbe wa ubongo na kusaidia tezi zinazoanza kuvimba, zitanywea kutokana na kuwapo zinki nyingi kwenye mbegu au mafuta ya maboga.

Mtaalamu huyo anatoa darasa lingine la kiafya kwamba kwa wanaotumia mafuta hayo kwenye chakula, mtiririko wake anatumia msamati 'moja kwa moja', akiunganisha na mfano wa dripu na sindano kwa mgonjwa, nafuu ikishuhudiwa kwa kasi na mtumiaji anaondokewa uchovu.

**MLONGE (MOLINGA)**

Kwa majani ya mlonge, yanatajwa kuwa na faida nyingi na katika mwili wa binadamu, yakiongoza kwa utoaji protini nyingi.

Majani hayo ya mlonge kwa baadhi ya makabila nchini hutumia kama mboga, hivyo kiafya yana hadhi sawa na mboga ya maharage, kwa utajiri wake wa protini nyingi.

Anataja ulaji mbegu za mlonge walau tatu kwa siku, anasema inasaidia kusafisha figo na kuweka sawa mifumo yake, kwa kuwa zinki an madini ya chuma kwa wingi kuliko vyanzo vingine asilia.

Pia, mafuta ya mlonge anayapa sifa, kusaidia kuondoa sumu katika figo na maini na kufanya mzunguko wa damu kuondoa uchafu wote, ikiwamo maradhi ya UTI (mkojo mchafu), hali kadhalika kupandisha kiweengo c ha kinga mwilini (CD4) kwa haraka, kwani mafuta hayo yana vitamin A na C nyingi.

**PARACHICHI, UBUYU, NYONYO**


Mtaalamu Twahir, analitaja kuwa tunda lenye uwezo wa kutoa mafuta mengi kwa matumizi ya kupaka, pia ni mbadala wa mafuta ya mzaituni (Olive).

Mafuta hayo yana virutubisho vya madini aina ya 'potassium' (madini ya chokaa), chuma, Vitamin A na E yenye faida kwa upande wa kuboresha afya ya moyo na kuleta unyororo wa ngozi na kuuweka uzee mbali sana.

Pia, anasema kokwa hizo anazozalisha zinatoa mafuta yanayotumika kwa vipodozi na urembo, zikiuzwa katika masoko ndani na nje ya nchi.

Anagusia mafuta ya nyonyo, yanasaidia kukuza nywele na kuondoa mba vichwani na inaimarisha afya ya ngozi, huku mashudu yanayopatikana baada ya kukamua mbegu za nyonyo, ikitumika kuzalisha mbolea nzuri kwa matumizi ya shambani.

"Natamani Watanzania sasa waendane na mabadiliko ya matumizi husunani ya mafuta wanayotumia katika maisha yao ya kila siku hasa katika ulaji, watumie mafuta ya matunda kwani nibora bora kuliko," anasisitiza Twahir,



Tunda parachichi na mbegu yake.



Jani la mlonge na mbegu zake.

AFYA

## UMRI WAKE KARNE NA ROBO...

# Hospitali Bombo; sasa mkombozi wa watoto 'njiti', kituo tiba viungo

**Na Cheji Bakari, TANGA**

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Tanga, Bombo, ni kati ya hospitali kubwa nchini zilizonufaika na maboresho kupitia Sekta ya Afya na Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Bombo, hospitali iliyojengwa tangu mwaka 1901, Tanganyika ikiwa chini ya utawala wa Ujerumani, hadi sasa imeshanufaika na maboresho kuanzia ngazi ya huduma, majengo, wataalamu bingwa wa magonjwa mbalimbali, pamoja na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa.

Tabibu bingwa wa tiba ya watoto hospitalini Bombo, Dk. Mohamed Salehe Abdallah, anazungumzia uwekezaji wa serikali kuhuduma afya ya mama na mtoto, kwamba unalenga kupunguzia vifo vya watoto, pia wanaozaliwa 'njiti'.



Dk. Abdallah anafafanua uwekezaji wa serikali ulivyo, kwamba unajikita kuwapatia mafunzo madaktari na wauguzi, sanjari na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa tiba katika vituo kwa madaraja yaliyo tofauti.

Sasa mtaalamu huyo anataja mafanikio yaliyofikiwa kwa Idara ya Watoto hasa wanaozaliwa 'njiti', kwamba kuna vifaa tiba vya kisasa vimesheheni, vikiwarahisishia wataalamu utoaji huduma eneo hilo la afya; Mama na Mtoto.

Dk. Abdallah anataja baadhi ya vifaa hivyo ni mashine za kisasa vinavyompatia mtoto 'njiti' joto, hewa safi na nyinginezo, ambazo awali hazikuwapo, akizitaja ni jitihada binafsi za Rais Dk. Samia.

Ni hatua inayofikiwa sasa, huku Julai mwaka jana (mwaka na mwezi mmoja uliopita), kulikuwapo hatua kubwa ya maendeleo, serikali ilipotangaza azma ya utiaji saini makubaliano inayoufanya mkoa wa Tanga kupitia Hospitali ya Rufani Bombo, kuwa Kituo Umahiri cha Kufanya Upasuaji wa Kurekebisha Viungo Nchini.

Akasema, urekebishaji huo wa viungo ni wa kumrejesha mtu kwenye hali yake ya kawaida na hivyo kuwa cha kwanza kwa ukanda wa Afrika Mashariki.

Aliyekuwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, ambaye ni Mbunge wa Tanga, akiwa hospitalini Bombo, akafafanua ni hatua inayolenga kumrudisha mtu viungo kwenye utendaji wake wa kawaida.

"Inasadikika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga -Bombo ndio ya kwanza nchini, ilijengwa na Wajerumani 1901, hivyo lazima tuipe hadhi yake... " ilifafanua taarifa ya mkoa wa Tanga inayoongeza kuwa mtazamo ni kupafanya kuwa Kituo cha Umahiri cha Upasuaji Kurekebisha Viungo Afrika Mashariki, kusaidia majukumu ya Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Katika azma hiyo, ufanikishaji wake uliangaza kwanza katika wataalamu kupata mafunzo ya umahiri, jukumu ambalo lilishirikisha mdau, Chuo Kikuu cha Beirut, Ujerumani.

### TAFSIRI YA NJITI

Mtaalamu Dk. Abdallah, anatoa darasa la mteja wake 'mtoto njiti' kwamba ni anayezaliwa kabla ya kutimiza umri wa miezi tisa na mara huzaliwa katika umri miezi saba.

"Huwa tuna kawaida ya kuangalia uzito wa mtoto, akiwa amezaliwa chini ya uzito tunaotegemea watoto wazaliwe nao tunasema huyo ni njiti," anfafanua.

Anaeleza kwamba kwa kawaida mtoto anapozaliwa, anatakiwa kuwa na uzito usiopungua kilo 2.5 huku mimba inatakiwa isipungue umri wa wiki 37 sawa na miezi tisa na inapotokea upungufu, hupatikana mtoto 'njiti'.

Kwa mujibu wa Dk. Abdallah, kama walivyo watoto wengine, wanazaliwa wakiwa hawajapevuka au kufikisha uzito unaohitajika.

Anafafanua, katika mustakabali huo, kuna mambo ya msingi yanazingatiwa kuwawezesha kuishi, ikiwamo kuwahifadhi katika 'kiotamizi' wapate joto linalotakiwa, pamoja na kuwaingizia hewa safi za kuwatanulia mapafu.

Dk. Abdallah anasema kupatikana kwa vifaa tiba hivyo na kuwapatia mafunzo wataalamu, kwa kiasi kikubwa imesaidia kupunguza idadi ya vifo vya watoto waliozaliwa kabla ya muda sahihi.



Mtaalamu Bingwa wa Afya ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Watoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga - Bombo, Dk. Mohamed Salehe Abdallah. **PICHA: CHEJI BAKARI**

"Serikali imeifanya Hospitali ya Bombo kufikia maendeleo makubwa kwa upande wa 'afya ya mama na mtoto' na napenda kutoa wito kwa wakazi wa mkoa wa Tanga kutumia fursa hiyo kuja Bombo, kwani ina madaktari bingwa wa watoto, wauguzi wazoefu na wenye weledi,"anatamka Dk. Abdallah

### KWANINI NJITI?

Bingwa huyo anafafanua sababu za wazazi kujifungua mtoto 'njiti', ni tatizo linaloambatana na sababu mbalimbali, ikiwamo maradhi yanayoshusha kinga za mwili kwa mjamzito, kuugua na lishe duni.

Pia, anataja mzazi kuwa ujauzito wenye zaidi ya mtoto mmoja yaani pacha, inaweka uwezekano wa mama kujifungua kabla ya kutimiza siku stahiki, msongo wa mawazo na nyenzo za kimwili za uzazi kuwa dhaifu.

Vilevile anaeleza kuwa mzazi wa njiti kuendelea kuwa na uzazi wa aina hiyo; ajali mbalimbali nazo zinamharakisha mtoto kuzaliwa kabla ya wakati; na mtindo wa maisha hususani kwenye lishe.

"Hapo zamani kinamama wajawazito walikuwa wanakula vitu vya asili vingi vikiwa na mlo kamili tofauti na ilivyo nyakati hizi, hivyo mama anatakiwa achukue tahadhari kutokana na sababu hizo pindi anapojihisi amebeba ujauzito," anaeleza.Kuhusu njia za kuzuia tatizo la kuzaa mtoto 'njiti', amesema kwa zipo njia ambazo zikitumiwa na mama mjamzito zinaweza kumsaidia kuepukana na tatizo hilo kama zilivyoelezwa hapo juu ispokuwa kuna sababu nyingine ambazo hazina namna ya kuepuka ni za kimaumbile ambapo amebainisha mama lazima aonane na daktari wa kinamama, kabla hajashika ujauzito.

"Hivyo, inashauriwa kwa kina mama kujenga tabia ya kuhudhuria kliniki za wajawazito ambazo huanza kipindi ambacho mimba ipo wiki ya 12 au miezi mitatu."

"Hata hivyo, inashauriwa ikiwa unapanga kupata mtoto kabla hujaanza taratibu za kupata mtoto uende kuonwa na daktari, ili kupata ushauri stahiki utakapotunga mimba inakuwa rahisi kufuatiliwa," anasema Dk. Abdallah.

Anafafanua kuwa, kitendo cha mjamzito kuhudhuria kliniki, kinamwezesha kujua lishe bora itakayomsaidia na anapopata mafunzo ya namna ya kujikinga na maradhi ya kuambukiza kama vile maambukizi katika njia ya mkojo (UTI), na yasiyoambukiza, kama kisukari, yanaweza kuathiri ukuaji wa mimba na afya ya mtoto akiwa tumboni.

Pia anataja elimu ya namna ya kujiandaa mpaka atakapofikia wakati wa karibu ya kujifungua na kufahamu vitu vinavyohitajika wakati wa kujifungua.





# Serikali kufunga kamera barabarani nchi nzima

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADA ya serikali kufunga mizani 78 nchini kwa ajili ya kudhibiti uzito wa magari, imetangaza lengo lake la kufunga kamera nchi nzima ili kudhibiti ajali.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Idara ya Usalama na Mazingira Wizara ya Ujenzi, Kashinde Musa, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani yanayofanyika kitaifa katika Uwanja wa Jamhuri jijini hapa.

Musa, alisema serikali imewekeza fedha nyingi katika ujenzi wa miundombinu ya barabara, moja ya changamoto iliyojitokeza ni uharibifu wa barabara kutokana na magari kubeba mizigo mizito zaidi ya uwezo wa barabara hizo.

"Niwatake wadau wote wa usafirishaji nchini kuhakikisha wanafuata taratibu na kanuni za uzito barabarani ili barabara zetu ziweze kudumu kwa muda ambao umekusudiwa," alisema.

Alisema wizara hiyo katika mwaka huu wa fedha wa 2024/25, imetenga bajeti kwa ajili ya kupunguza msongamano wa magari katika barabara za majiji ya Arusha, Dodoma, Mwanza, Mbeya na Dar es Saalam.

"Mradi huu utakapokamilika tunatarajia utasaidia kupunguza ajali katika maeneo hayo, lakini lengo letu ni kuhakikisha mradi huu unakwenda nchi nzima," alisema.

**"Niwatake wadau wote wa usafirishaji nchini kuhakikisha wanafuata taratibu na kanuni za uzito barabarani ili barabara zetu ziweze kudumu kwa muda ...**

Musa aliendelea kusema kuwa, wizara hiyo imejikita katika matumizi ya teknolijia za kisasa kwa ajili ya kupunguza ajali nchini, ikiwamo ufungaji ...kamera za usalama barabarani.

"Kuna mradi wa majaribio wa ufungaji wa kamera ambao tuliufanya katika mikoa ya Pwani na Morogoro mwaka 2016 tumebaini tangu wakati huo, ajali zimepungua kwa kiasi kikubwa, hivyo lengo letu ni kufunga kamera hizo nchi nzima," alisema.

Aliitaja changamoto nyingine inayoikabili wizara hiyo kuwa ni uharibifu na wizi wa alama za usalama barabarani na kusababisha ajali.

"Tunaweka alama za barabarani, lakini wizi wa alama hizo ni tatizo, tumekuwa tukitoa elimu kwa wananchi kuacha kufanya hivyo. Aidha, wanaobainika hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi yao," alisema.

Meneja wa Mazingira na Jamii, Wakala wa Barabara nchini (TANROAD), Zafarani Madayi, alisema kila mtu ana wajibu wa kutunza miundombinu ya barabara.

Madayi, alisema wananchi wanapaswa kutunza miundombinu ya barabara na kuacha kufanya shughuli za kibinadamu kwenye hifadhi ya barabara.

"Sheria inakataza watu kufanya shughuli yoyote ya kibinadamu katika hifadhi ya barabara na kwa mujibu wa sheria eneo la hifadhi ya barabara ni mita 60, yaani mita 30 kila upande," alisema.

Aliwataka wananchi kuacha kuchoma moto miti na nyasi kwenye maeneo ya barabara na kupitisha mifugo ili kunusuru kingo za barabara kumeguka na kuharibika kwa muda mfupi.

## TAKUKURU yataka jamii kuepuka rushwa uchaguzi wa mitaa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani hapa, Victor Swella, ameitaka jamii kuepuka kupokea rushwa ya fedha na kanga wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa ili wachague viongozi bora watakaoleta maendeleo.

Swella alitoa wito huo wakati akitoa elimu kuhusu kupinga rushwa kwa mashirika yasiyo ya kiserikali (AZAKI) jijini hapa.

Alisema hakuna sababu ya wananchi kukubali kurubuniwa kwa fedha na kanga, wanachotakiwa ni kuwa na msimamo wa kumchagua kiongozi bora wa kuwaletea maendeleo.

"Naomba wananchi tuisaidie serikali kupiga vita rushwa ili tuchague viongozi wanaostahili kuiongoza jamii katika maeneo mbalimbali nchini," alisema Swella.

Alisema imekuwa desturi ya wagombea kurubuni wananchi kipindi cha uchaguzi ili wawachague wakati hawana sifa yoyote.

Alionya kuwa, waliopanga kutoa rushwa wakati wa uchaguzi, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao wakibainika.

Aliwaomba wananchi kutoa taarifa kwa taasisi hiyo kwa watakaojihusisha na vitendo hivyo katika uchaguzi huo utakaofanyika Novemba mwaka huu.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (wa pili kulia) na Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Fatma Nyangasa (wa pili kushoto), wakikata utepe kuzindua tamasha la saba la siku tatu la jinsia, lililoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), wilayani humo, juzi. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya TGNP, Igemma Akilimali na Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao huo, Lilian Lihundi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwanasheria Mkuu mpya ala kiapo bungeni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali (AG), Hamza Johari, amekula kiapo cha uaminifu mbele ya Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson.

Johari, alikula kiapo hicho muda mfupi kabla ya kuanza kikao cha kwanza cha Mkutano wa 16 Bunge la 12 jijini hapa.

Aliapishwa kwa mujibu wa Ibara ya 59 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inayompa mamlaka ya kuwa mbunge na kuhudhuria vikao vya Bunge.

Baada ya kula kiapo, mwanasheria huyo mkuu wa serikali, alikabidhiwa nyaraka za kumwezesha kufanya kazi akiwa Bungeni na Spika.

Kiapo hicho cha uaminifu mbele ya Bunge kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kinafuatia uteuzi uliofanywa na Rais wa Samia Suluhu Hassan Agosti 15, mwaka huu na kuapishwa Agosti 16 Ikulu jijini Dar es Salaam.

Johari aliteuliwa kuwa AG baada ya Jaji Dk. Eliezer Mbuki Feleshi aliyekuwa akishikilia wadhifa huo kuteuliwa na Rais Samia kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani.

Kabla ya uteuzi huo, mwanasheria huyo mkuu wa serikali alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga nchini (TCCA).



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kerezange, Job Ndubussa (katikati) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Sustainology, Ansh Shah (kulia), pamoja na Ofisa Mtendaji Mkuu wa BR Food Industries, Colin Francis, wakishirikiana kupanda moja kati ya miti 200 ya kahawa shuleni hapo, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti 5,000,000 ya zao hilo, ambapo itapandwa mkoani Kagera. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# WASH yatajwa kuwa mkombozi homa ya nyani

**Na Jenifer Gilla**

WATANZANIA wameshauriwa kuzingatia njia za matumizi ya maji salama, usafi wa maji na mazingira (WASH) ili kudhibiti maambukizi ya ugonjwa wa homa ya nyani unaoisumbua nchi jirani.

Aidha, serikali imesema imejizatiti kukabiliana na ugonjwa huo nchini, kupitia njia mbalimbali ikiwamo kuimarisha utoaji wa huduma ya afya na elimu kwa umma.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki iliyopita katika mdahalo uliofanyika kupitia mtandao wa kijamii wa X uliolenga kutoa elimu kwa umma kuhusu ugonjwa huo.

Mwenyekiti wa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mabadala, Prof. Hamisi Malebo, alisema ugonjwa huo unaweza kudhibitiwa kwa zaidi ya asilimia 60 kama jamii itazingatia matumizi ya WASH, yakihusisha kunawa na maji safi na matumizi ya vitakasa mikono.

Alisema mtu aliyepata maambukizi anapaswa kunawa kwa maji safi na salama au kutumia vitakasa mikono mara kwa mara, ili kuua vimelea na kupunguza maambukizi kwa watu wengine.

Prof. Malebo alishauri wagonjwa hao kuosha malengelenge au vidonda kwa kutumia maji yenye chumvi inayojulikana kitaalam kama 'baking' soda, Epsom na 'potassium permanganate' ili kuua virusi na kuponya kwa haraka vidonda hivyo.

"Wagonjwa waepuke kujikuna vipele hivyo kwa sababu vikipasuka yale majimaji yanasambaza ugonjwa huo zaidi na wanashauriwa kunawa kwa maji safi na sabuni na kuhakikisha kuwa vile vifaa walivyotumia kama vile nguo na vyombo visafishwe na ili kuua vimelea," alisema.

Prof. Malebo alishauri wale wanaohudumia au kuwaona wagonjwa wavae barakoa, 'gloves' na baadaye kuzichoma na kusafisha kwa vitakasa mikono maeneo yote wanayohisi mgonjwa alishika.

Alishauri wamiliki wa vyombo vya usafiri wa umma kama vile daladala wasafishe magari yao kwa vitakasa hasa sehemu zinazoguswa kama vile kwenye mabomba, ili kuuwa virusi kwa kuwa vinaweza kukaa nje ya mwili wa binadamu kwa muda mrefu kama hakutakuwa na joto linalozidi nyuzijito 50.

"Hata watumiaji wa daladala warudishe utaratibu wa kutumia vitakasa mikono mara wanaposhuka katika usafiri huo, ili kama walipata virusi waviteketeze na kujiepusha na maambukizi," alisema.

> **"Wagonjwa waepuke kujikuna vipele hivyo kwa sababu vikipasuka yale majimaji yanasambaza ugonjwa huo zaidi na wanashauriwa kunawa kwa maji safi na sabuni na kuhakikisha kuwa vile vifaa walivyotumia...**

Alishauri pia maeneo yote yenye mikusanyiko ya watu kama vile ofisini, sokoni na mabenki kurudishwe utaratibu wa kutumia vitakasa mikono na maji ya kunawa ili kupunguza maambukizi.

Aidha, alisema kwa sasa kuna visa 5,199 duniani kati ya hivyo 1,854 vimetokea Bara la Afrika na visa 1,754 sawa na asilimia 95 vinatoka katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Elimu ya Afya kwa Umma, Wizara ya Afya, Dk. Norman Jonas, alisema kwa kiasi kikubwa ugonjwa huo unasababishwa na migusano ya moja kwa moja kupitia ngozi na kugusa majimaji ya mwilini kama vile damu, matapishi ya mtu aliyeathirika.

Alisema pia huweza kuambukizwa kwa kugusa vitu ambayo vimeguswa na mtu aliye na mambukizi kama vile vitasa vya mlango, nguo na huweza kuishi kwenye hivyo vitu kwa muda mrefu.

Pia huweza kuambukizwa kutoka kwa mnyama kwenda kwa binadamu kupitia shughuli za kibinadamu kama vile uwindaji, kung'atwa na mnyama au mdudu aliyeambukizwa na kula nyama yenye maambukizi na mama mjamzito kumwambukiza mtoto aliyetumboni.

Dk. Jonas alishauri mtu akihisi kuwa na dalili za ugonjwa huo kuwahi kituo cha kutolea huduma za afya kilichopo karibu yake au kupiga simu namba 199 bure, ili kupata tiba ya awali na kuilinda jamii inayokuzunguka.

Alisema Wizara ya Afya inashirikiana kwa karibu na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kutoa elimu kwa umma juu ya ugonjwa huo kupitia vyombo vya habari, ili kuhamasisha na kushirikisha jamii kukabiliana na ugonjwa huo.

Alisema mpaka sasa wameandaa vielelezo 64 ikiwamo vipeperushi na ujumbe wa video zaidi ya 43, wamefanya vipindi zaidi ya 37 vya luninga na redio za kijamii na kitaifa na magazeti, matamko ya viongozi ikiwamo Waziri wa Afya na mabango ya matangazo barabarani.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Kuambukiza KCMC, Dk. Elinchilia Shao, alisema kuwa dalili za msingi za ugonjwa huo ni homa kali, vipele vikubwa vinavyobonyea katikati, vyenye milimita mbili hadi tano na vinavyouma, misuli kuuma na kupata mitoki.

"Kuwapo vipele vile pia kunatokana na kirusi kimeingilia wapi, kama kimeingilia mdomoni basi utapata vipele eneo hilo ingawa wengi hupata usoni," alisema.

Alisema wagonjwa wanaotumia dawa za kuongeza kinga ya mwili kama vile wanaoishi wa Virusi vya UKIMWI, huchukua muda mrefu kuonyesha dalili hivyo wanaweza kuambukiza wengine bila wenyewe kufahamu kama wana ugonjwa huo.

Alisema pia dalili hizo zinatofautiana kulingana na umri wa mtu, watu wazima wanapata dalili kidogo ukilinganisha na watoto kwa kuwa walishapata chanjo ya ndui ambayo inahusiana na ugonjwa huo.

Mkurugenzi wa Huduma za Tiba Magonjwa ya Dharura na Maafa Wizara ya Afya, Dk. Erasto Sylvanus, alisema kwa sasa kuna namna ya kumtibu mgonjwa anatibiwa kulingana na dalili alizonazo, kama anahoma atapewa dawa za kushusha homa na kumsaidia vipele visiwashe na kusambaa zaidi, kumpa maji ya kutosha na lishe nzuri vyakula pamoja na kumtenga ili asiambukize wengine.

Dk. Erasto alisema wizara ya afya inahakikisha kuwa inafuatilia tetesi izote za wahisiwa wa kuwapo na wagonjwa huo katika maeneo mbalimbali, ikiwamo mipakani kwenye viwanja vya ndege na vituo vya kutoa huduma za afya za ngazi zote ili kuchukua hatua stahiki.

## Bunge lataka serikali kufuatilia katazo dola biashara ya tumbaku

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ameitaka serikali kufuatilia katazo lake lililotolewa katika Mkutano wa 15 wa Bunge la Bajeti la kuzuia matumizi ya Dola ya Marekani ili kulinda shilingi isiporomoke kama lilijumuisha biashara ya tumbaku.

Kauli hiyo ya Spika Tulia ilitokana na majibu ya serikali bungeni jana katika swali la Mbunge wa Tabora Kaskazini (CCM), Almas Maige, aliyejenga hoja kwamba biashara yote ya tumbaku inafanyika kwa dola, hivyo kuhoji kwanini wakulima wanalipwa kwa Shilingi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, alisema biashara hiyo inafanyika kwa dola isipokuwa uhamishaji malipo kutoka kwa mnunuzi kwenda katika vyama vikuu vya msingi hufanyika kwa dola.

Silinde alisema katika vyama vya msingi baada ya makato yote, ikiwamo wakulima wanayokuwa wamekopa katika msimu wa kilimo na fedha inayobaki, wakulima wanalipwa kwa Shilingi kulingana na thamani ya fedha ya siku husika.

Kutokana na majibu hayo, Spika Tulia alihoji nani anayebadilisha katika biashara hiyo ikiwa mkulima anapata pembejeo kwa dola na mnunuzi ananunua kwa dola.

Silinde alifafanua kuwa chama kikuu cha msingi kimeingia mikataba na wakulima na akaunti za wakulima ni za Shilingi na wanachokifanya hulipa kwa kuzingatia thamani ya dola ya siku hiyo.

Hata hivyo, Spika Tulia alitaka kujua kuhusu katazo la serikali la matumizi ya dola kama lilizingatia biashara ya tumbaku ili kulinda Shilingi isiporomoke.

"Lilitoka katazo hapa bungeni na Waziri wa Fedha la matumizi hayo yaondolewe, sasa mbona serikali katika majibu yenu, inaonekana kama mnatia moyo, lakini fuatilieni katazo lenu wenyewe kuhusu mkulima kukopeshwa kwa dola na kulipwa kwa dola na hapo katikati kugeukiwa na kulipwa Shilingi.

"Sikumbuki vizuri kama lile katazo liliwekwa katika sheria ya fedha au halikuwekwa na kama iliwekwa, haya majibu mliyotoa itakuwa ni makosa, lakini kama hatukuweka ni jambo la kuanza kufikiri kulitatua," alisema.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Ulyankulu (CCM), Rehema Migila, alihoji sababu zipi zinachangia wakulima wa tumbaku kukopeshwa pembejeo na kuuza tumbaku kwa dola badala ya Shilingi ya Tanzania.

Naibu Waziri Silinde akijibu swali hilo, alitaja sababu nne zinazofanya kuwa na utaratibu wa wakulima wa tumbaku kukopeshwa pembejeo na kuuza tumbaku kwa Dola za Marekani na kulipwa kwa dola unatokana sababu za msingi.

Alisema sababu ni biashara hiyo kuwa ya kimataifa hufanyika kwa Dola ya Marekani kuanzia upatikanaji pembejeo, ugharamiaji uzalishaji hadi uuzaji; uuzaji wa tumbaku kwa dola unamlinda mkulima na hasara ambazo zinatokana na mabadiliko ya Shilingi na kumhakikishia uimara wa kipato chake.

"Zao la tumbaku linaendeshwa katika misingi ya biashara ya mikataba inayosimamia ubora, madaraja na taratibu zake hadi inapofikishwa katika soko na hupimwa kwa viwango vya Kimataifa," alisema.

Alisema mfumo huo unaihakikishia nchi upatikanaji wa dola na usimamizi rahisi wa fedha za mauzo kurudi ndani ya nchi.

"Mfano, msimu wa 2022/2023, wakulima wa tumbaku walilipwa Dola za Kimarekani milioni 286.8 na taifa letu lilipata dola milioni 480, kutokana na kuzalisha na kuuza tani 122.8 za tumbaku nje ya nchi na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya pili kwa Afrika, katika uzalishaji na mauzo ya tumbaku nje ya nchi,"alisema.



# Mwinyi aeleza matarajio yake TASAF

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ni matarajio yake Mfuko wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF) utaendelea kuboresha maisha ya kaya maskini kwa kuzitoa katika mazingira magumu kwa kuinua kipato na uchumi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar wakati akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko huo, Shedrack Salmin Mziray, baada ya kwenda kujitambulisha baada ya kuteuliwa na Rais Samia kushika wadhifa huo hivi karibuni.

Alisema anatarajia miradi ya TASAF kwa kaya maskini nchini itaendelea kuzisaidia kaya zilizo kwenye mazingira magumu kwa lengo la kuzitoa uko.

Mwinyi alipongeza uongozi wa TASAF kwa kuboresha maisha ya familia 22,000 Zanzibar kupitia miradi 15 yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.1 ikiwamo vituo vya afya, madarasa, majisafi na salama na barabara za vijijini.

Alisema mfuko huo, pia umesaidia kukuza uchumi wa wananchi, kuongezea kipato kwa kaya masikini na ajira ndogondogo.

Alipongeza mpango wa TASAF awamu ya pili kwa kuendelea kusaidia maeneo ambayo serikali bado haijakamilisha.

Mziray, alisema kwa sasa TASAF inatekeleza kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya miradi yake tangu mwaka 2020 hadi kukamilika kwake Septemba mwakani.

Mziray aliteuliwa kushika wadhifa na Rais Samia Julai 3, mwaka huu, baada ya aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa mfuko huo, Ladislaus Mwamanga kustaafu.

Kabla ya uteuzi huo, Mziray alikuwa Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani wa TASAF.

# SMZ yasisitiza kusimamia mradi wa Pemba ya Kijani

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imesisitiza kuwa itasimamia utekelezaji wa Mradi wa Kijani (SASA) katika Kisiwa cha Pemba ili kulinda mazingira na kuboresha huduma bora kwa wananchi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar, Shamata Shaame Khamis, wakati akizindua mradi huo jana katika Uwanja wa Madungu Chakechake kisiwani humo.

Khamis, alisema mradi huo unatakiwa kutekelezwa haraka kwa vile utasaidia upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi.

Alisema mradi hupo pia utasaidia ukarabati wa shule 19, vituo vya afya 10, kuwawezesha wajasiriamali wadogo, kinamama wanaolima mwani kupata mafunzo na mikopo kwa masharti nafuu na usimamizi wa usafi wa mazingira katika miji.

" Tuhakikishe mradi huu tunautekeleza kwa malengo tuliyoyakusudia na serikali inaendelea kuthamini michango ya washirika wa maendeleo wa ndani na wa nje, wakiwamo Umoja wa Ulaya (EU) na kuahidi kushirikiana ili kufanikiwa zaidi," alisema.

Khamis, alisema EU imetoa misaada ya utaalamu, fedha na nyenzo tofauti nchini kwa ajili ya kufanikisha mradi huo.

Alisema tangu mwaka 1975 wamechangia zaidi ya Euro bilioni mbili kwa maendeleo nchini kupitia miradi mbalimbali.

Naibu Katibu Mkuu Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ, Mikidadi Mbarouk Mzee, alisema Euro milioni 75 zimetolewa baada ya kuingia mikataba miwili ya ruzuku kwa ajili ya mabadiliko katika vitongoji vya mijini kwa Pemba kwa kuimarisha ustahamilivu wa miji.

"Tunaishukuru EU kwa msaada wa fedha za uchumi wetu ikiwamo katika maeneo ya uchumi wa buluu na mabadiliko ya hali ya hewa, udhibiti na mageuzi ya taasisi, mpango wa ukuaji wa mitaji kwa wajasiriamali kwenye kilimo na utawala, ukusanyaji wa takwimu za jinsia na udhibiti wa kazi za nishati," alisema.

**"Nina furaha kusherehekea nanyi katika uzinduzi wa miradi hii na ninasisitiza dhamira yetu ya kufikia matokeo chanya yatakayoonekana hivi karibuni," alisema.**

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, alisema wamefarijika kupata mradi huo na kuahidi kushirikiana na kuunga mkono jitihada hizo kwa kufanya usimamizi na ufuatiliaji.

Mkurugenzi wa Mradi huo, Martino Vinci, alisema unalenga kuboresha miundombinu ya mijini, kuimarisha huduma za msingi kama vile usimamizi wa majisafi na majitaka, kuibua fursa za kiuchumi kwa vijana, wanawake katika sekta kilimo cha mwani na kuchakata taka.

"Nina furaha kusherehekea nanyi katika uzinduzi wa miradi hii na ninasisitiza dhamira yetu ya kufikia matokeo chanya yatakayoonekana hivi karibuni," alisema.

Mtekelezaji wa mradi huo kutoka Shirika la Msaada ya Ubelgiji (ENABEL), Koenraad Goekint, alisema utaboresha ufanisi wa kazi katika taasisi zao, mazingira wanayoishi na maisha ya familia, watoto, vijana na wanawake.

"Katika mwaka mmoja au miwili ijayo tunatarajia kuona shule zikiwa na hali bora kwa watoto, jamii zikiwa na maeneo ya umma yaliyoboreshwa, upungufu wa taka, usambazaji bora wa maji na usafi wa mazingira," alisema.

Balozi wa EU nchini, Christine Grau, alisema hiyo ni fursa muhimu kwa wakazi wa Pemba kuwa na mazingira bora na hewa safi ya kuvutia.

Mradi huo unaendeshwa na wizara hiyo kwa ufadhili wa EU, pia unatekelezwa katika mikoa ya Tanga, Mwanza.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na Uongozi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF), ukiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Uongozi ya Mfuko huo, Peter Ilomo (wa tatu kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji, Shedrack Mziray (wa pili kushoto), Ikulu Zanzibar, juzi. **PICHA: IKULU**

# Wafanyabiashara, wakulima wa karafuu wapewa somo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAFANYABIASHARA na wakulima wa zao la karafuu kisiwani Pemba wametakiwa kufuata utaratibu uliowekwa na serikali ili kuondokana na usumbufu wakati wa malipo.

Waziri wa Biashara na Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaban, alisema mapato yanayotokana na karafuu yamechangia kuleta maendeleo nchini, hivyo ni vyema kulipa zao hilo kipaumbele.

Akizungumza jana kisiwani humo katika hafla ya kugawa zawadi kwa wakulima walioibuka washindi wa pikipiki, baiskeli na simu, alisema serikali inashirikiana na Kampuni ya Tigo-Zanztel kuhakikisha wananchi wanapata stahiki zao kutokana na zao hilo.

"Hivi sasa mifumo inayotumika katika malipo ya karafuu kwa wakulima na wafanyabiashara ni mifumo ya kisasa na tumeachana na mfumo wa zamani ambao unaweza kuwakwamisha katika utekelezaji wa shughuli zetu," alisema Omar.

Alisema serikali inajitahidi kulipa kipaumbele zao hilo kwenye mauzo kupitia nchi mbalimbali ili ipate mapato na kuboresha huduma kwa jamii.

Waziri huyo, aliwataka wafanyabiashara wa zao hilo kuongeza uzalishaji na kuacha tabia ya kukata mikarafu, vingine wanaua rasilimani iliyopo kisiwani humo.

"Pemba kuna fursa mbalimbali hivyo wananchi mnatakiwa kuunga mkono juhudi za serikali katika kuleta maendeleo kwa wananchi wake na kila mmoja ana wajibu wa kulinda fursa hizi waweze kufaidika nazo," alisema.

Mkurugenzi wa TigoZanztel, Aziz Said Ali, alilishukuru Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar (ZSTC) kwa kuendelea kuwaunga mkono kutoa huduma kwa wananchi hususan wafanyabiashara wa karafuu.

Ali, alisema watahakikisha wanaisadia serikali kuwaletea maendeleo wananchi kwenye miundombinu ya mawasiliano katika kipindi hiki ambacho dunia iko kwenye mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Alisema azma ya serikali kukifungua Kisiwa cha Pemba kwenye sekta ya biashara na viwanda ni kuwaboreshea wafanyabiashara mazingira ya biashara na kuongeza kipato.

"Wafanyabiashara tunawaomba mwendelee kuuza karafuu zenu katika vituo ambavyo vinastahili, ambavyo vipo katika usimamizi wa Shirika la Biashara la Zanzibar, kwani serikali imeboresha mpango wa usafirishaji kupitia Bandari ya Mkoani," alisisitiza.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**WIZARA YA ARDHI,NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MASWA. LILILOPO MASWA.**

**MAOMBI MAKUBWA NA.21 YA MWAKA 2024**

**KATI YA MALOBA BUSUMABU MANYENYE.......MLETA MAOMBI (As the administrator of the Estate of the late Maduhu Lushanga Mkungu)**

**DHIDI YA**

1. **BULUGU DANGA**
2. **LUSHANGA MADUHU .........................WAJIBU MAOMBI**

**WITO/TAARIFA**

**Kwa: LUSHANGA MADUHU POPOTE ALIPO KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua Maombi dhidi yako katika Baraza hili la wilaya ya Maswa,maelezo ya madai yanaweza kupatikana hapa Barazani.Unatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wako wa maandishi kabla ya tarehe 26.09.2024.

Pia unajulishwa kuwa shauri hili limepangwa kutajwa siku ya tarehe 26.09.2024 saa 2;30 asubuhi mbele ya Mhe.J.T.Kaare Mwenyekiti,Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Maswa.

Na pia unafahamishwa kuwa iwapo utakadi wito huu na kushindwa kuleta utetezi wako wa maandishi kwa muda uliopangwa,Baraza litalazimika kusikiliza shauri hili upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.

IMETOLEWA kwa MKONO wangu na MHURI wa Baraza hili leo tarehe 15.08.2024

J.T.KAARE
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MASWA

---

## TANGAZO

Mimi **GEDIOSE RWEYEMAMU** natafuta rafiki zangu Ndugu **MR STANLEY T MARIKI** na **MRS. JENEROSE KABULA MARIKI** ambao sijaonana nao siku nyingi . Popote walipo tuwasiliane kupitia namba **0692945649 au Email gediose@hotmail.com**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JORAM LUCHEMO MANGATI**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 250EEG,** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**PHQ/MOR/MOR/28534/2024**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**

**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 19987 YA MWAKA 2024.**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU JUSTIN MOSHA SEKUMBO**
**NA**
**CLARA JUSTIN SEKUMBO ............................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa maombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 25 mwezi Tisa,2024 saa 8:00 asubuhi, siku ambayo shauri hili limepangwa kusikilizwa mbele ya Mhe Jaji A.A OMARI.

Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 26 Mwezi wa nane, 2024

NAIBU MSAJILI

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 20854 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late DONASIAN ROGASIAN PATRICE**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY REVINA ERNEST KUSAGA @REVINA DONASIAN**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the 27th Day of SEPTEMBER, 2024

Dated at Dodoma this 20th Day of AUGUST, 2024.

Presented for filing this 28th day of AUGUST 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA PIKIPIKI NA KADI YA PIKIPIKI

**HEIFER PROJECT INTERNATIONAL TANZANIA** anatangaza kupotelewa na PIKIPIKI na KADI YAKE aina ya **LIFAN LF-150** zenye usajili namba **MC468CYR,** CHASSIS: **LFGT150GN000196** na ENGINE NAMBA: **LF162FMJGTK000196,** Mahali: Kijiji cha Mbwade, kata ya Madoto, Wilaya ya Kilosa. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/MWA/ILE/24939/2024,**
**KMB/RB/1532/2021**

---

## KUPOKEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HEIFER PROJECT INTERNATIONAL TANZANIA** anatangaza kupotelewa na KADI YA PIKIPIKI aina ya **LIFAN LF-150,** yenye usajili namba **MC473CYR,** CHASSIS NAMBA: **LFGT150GN000184** na ENGINE NAMBA: **LF162FMJGTK000184** ,Mahali: Nronga Miaseni, Kilimanjaro. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA :
**PHQ/MWA/ILE/18364/2024**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 15571 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late of the late HAFSI ENOCK MALAMBATI of Iyumbu Within Dodoma City.**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ESNATH KEPHA CHILOBE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 10 Day of 09, 2024

Dated at Dodoma this 07 Day of 08, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: +255 - 745 700 710.***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Aliyechanganya udongo wa Muungano afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

MMOJA wa watu waliochanganya udongo wakati Tanganyika na Zanzibar zinaungana mwaka 1964, Omar Hassan Mkele (75), amefariki dunia.

Mkele alikuwa mmoja wa Watanzania wanne walioshiriki kuchanganya udongo huo na alizaliwa mwaka 1949 na wakati huo alikuwa na umri wa miaka 15.

Maziko ya Mkele, aliyefariki dunia jana, yalifanyika jana Kibweni, Uwanja wa Mpira, Zanzibar na kuhudhuriwa na viongozi na wananchi mbalimbali wakiongozwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Kabla ya maziko hayo, Dk. Mwinyi alijumuika na waumini wa dini ya Kiislamu katika sala ya maiti kwenye Msikiti wa Kibweni Mshelishelini, Wilaya ya Magharibi A, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Baada ya maziko, Dk. Mwinyi alifika myumbani kwa marehemu kuwafariji na kuwapa pole wafiwa na kuwataka kuwa na subira wakati wa msiba huo mzito.

Miongoni mwa viongozi walioshiriki maziko hayo ni pamoja na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla, Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Saidi Dimwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu, Ali Suleiman Ameir na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Hamza Hassan Juma.

**Kabla ya maziko hayo, Dk. Mwinyi alijumuika na waumini wa dini ya Kiislamu katika sala ya maiti kwenye Msikiti wa Kibweni Mshelishelini, Wilaya ya Magharibi A, Mkoa wa Mjini Magharibi**

# Namibia yashikilia meli iliyobeba vifaa vya kijeshi kwenda Israel

**WINDHOEK,** Namibia

NAMIBIA imeishikilia meli inayoshukiwa kubeba shehena ya zana za kijeshi vilivyokusudiwa kutumiwa katika vita vinavyoendelea Ukanda wa Gaza.

Waziri wa Sheria wa Namibia, Yvonne Dausab, aliviambia vyombo vya habari vya serikali kuwa meli hiyo ilisimamishwa na kulazimishwa kutia nanga katika bandari moja nchini humo kutokana na kubainika kubeba vifaa vyenye vilipuzi vinavyopelekwa Israel.

Meli hiyo inayoitwa MV Kathrin, ilianza safari kutoka Vietnam, ilikuwa imeomba ruhusa ya kutia nanga katika bandari ya Walvis Bay, kabla ya kuelekea kaskazini kwenye njia inayoshukiwa kuelekea Mediterania kupitia Mlango Bahari wa Gibraltar.

Mashirika ya kutetea haki za binadamu yalikuwa yameonya kwamba Namibia ingeweza kuhusishwa na ukiukaji wa haki za binadamu kama ingeruhusu meli hiyo kutia nanga.

Haijajulikani ni kwa nini meli hiyo ilitaka kutia nanga katika nchi hiyo, lakini vyombo vinavyosafiri kwa muda mrefu huwa vinasimama ili kupata mahitaji muhimu kwa kipindi hicho, ikiwamo kupumzika, kupakua au kubeba mizigo.

Desemba mwaka jana, nchi ya Afrika Kusini ilifungua kesi ambayo inaendelea kusikilizwa katika Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ) ikidai Israel inafanya mauaji ya kimbari dhidi ya Wapalestina katika Ukanda wa Gaza.

Hata hivyo, Israel imekanusha madai ya kufanya mauaji ya halaiki na kusema kuwa kesi hiyo haina msingi.

Mzozo huo ulianza baada ya Hamas kuanzisha shambulio ndani ya Israel Oktoba 7, mwaka jana na kuua watu 1,200 na wengine 251 kuchukuliwa mateka.

Wakati huo huo, Wapalestina 11 wameuawa na wanajeshi wa Israel walipovamia eneo la kaskazini mwa Ukingo wa Magharibi unaokaliwa kwa mabavu.

Maofisa wa afya wa Palestina, waliripotiwa kuwa watu hao waliuawa katika shambulizi la anga kwenye kambi ya wakimbizi ya al-Far'a.

Vikosi vya usalama vya Israel vilisema vinafanya operesheni ya kukabiliana na ugaidi katika eneo la Jenin na Tulkarm.

Operesheni hiyo imetajwa kuwa kubwa kufanywa na Israel ndani ya Ukingo wa Magharibi na kuhusisha miji minne ya Jenin, Tulkarm, Nablus na Tubas.

Ripoti za Wapalestina zilisema kuwa, barabara kuu za kuelekea Jenin zilifungwa kutokana na mapigano yenye kuhusisha silaha katika kambi ya wakimbizi ya mji huo.

Wanajeshi wa Israel walisemekana kuingia katika hospitali moja huko Jenin na kuwazuia watu wawili huko Tulkarm.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Israel, Israel Katz, alisema kuwa, Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) limekuwa likifanya kazi kwa nguvu zote tangu jana usiku katika kambi za wakimbizi za Jenin na Tulkarm ili kubomoa miundombinu ya kigaidi ya Iran na makundi ya Kiislamu yaliyoanzishwa.**BBC**



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhajj Dk.Hussein Ali Mwinyi, akibeba jeneza likiwa na mwili wa Hassan Omar (Mkele), mmoja wa Watanzania aliyebeba udongo wa Muungano kati ya Zanzibar na Tanganyika, kabla ya kuanza kwa sala ya maiti iliyofanyika katika Msikiti wa Kibweni, Wilaya ya Magharibi "A" Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# Mvutano mkali kesi Uchaguzi wa Mitaa

**Na Grace Gurisha**

MVUTANO wa kisheria umeibuka mahakamani kuhusu kesi ya kupinga Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kusimamiwa na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Kutokana na mvutano huo, Mahakama Kuu Masjla Kuu Dar es Salaam inatarajia kusikiliza mapingamizi manne yaliyowasilishwa na serikali katika shauri hilo la kikatiba lililofunguliwa na wanaharakati watatu kupinga TAMISEMI kusimamia uchaguzi huo.

Vilevile, mahakama hiyo imeongeza muda wa siku zingine 14 kusikiliza shauri hilo ambalo muda wake ulikuwa umeisha kufikia jana kisheria. Kanuni zinataka rukhsa ya kuleta maombi ya mapitio ya kimahakama isikilizwe na kutolewa uamuzi ndani ya siku 14.

Mahakama hiyo ilifikia uamuzi huo jana mbele ya Jaji Wilfred Dyansobera baada ya Wakili wa Serikali Mkuu kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Marck Rwambo kueleza mahakama kwamba wana mapingamizi manne, ikabidi pande zote ziwasilishe hoja zao.

Jaji Dyansobera alisema amezingatia hoja za pande zote mbili katika suala la muda, na kwa mamlaka aliyopewa anaongeza muda wa kusikiliza shauri hilo kwa kuzingatia maombi yamewasilishwa kwa hati ya dharura.

"Shauri hili haliwezi kusikilizwa kwa siku 14 likaisha, litasikilizwa kwa kuunganishwa kwa maombi na mapingamizi, itasaidia kuendana na muda," alisema Jaji Dyansobera.

Alisema ni kweli siku hizi kuna mfumo wa kielektroniki na mahakama inajua changamoto za kufaili kwenye mfumo, kwa hiyo hoja ya mawakili ya kutaka kufaili leo (jana) inaweza isiwezekane kutokana na mtandao kusumbua.

"Kwa hiyo, mahakama inaona na kueleza kwamba leo (jana) waleta maombi wawasilishe kiapo kinzani na wafuatilie na kuzipitia vizuri kuanzia Ijumaa, Jumamosi na Jumapili ili mjiandae vizuri Jumatatu tunasikiliza," alisema Jaji Dyansobera.

Alisema anaweza akapanga siku ya Ijumaa kusikiliza mambo yasikamilike kutokana na mfumo wa kufaili uliopo.

Awali Rwambo alidai kuwa wakati wanaandaa majibu ya kiapo kinzani, wamebaini kuna masuala ya kisheria ambayo mahakama inapaswa iyafanyie kazi kwanza ndipo kesi ya msingi iendelee kusikilizwa.

Alidai kutokana na hali hiyo, wamewasilisha mapingamizi manne ya awali, hivyo aliomba mahakama ianze kusikiliza mapingamizi hayo na kama mahakama itakubaliana nayo, kesi itaishia hapo, na isipoyakubali, kesi itaendelea.

"Tusipoteze muda wa mahakama, mapingamizi haya yanaweza kumaliza shauri, ikiwa itayakataa basi shauri litaendelea kusikilizwa na mahakama kutoa uamuzi," alidai.

Akijibu hoja hizo, Wakili wa wanaharakati hao, Mpare Mpoki alidai hawezi kusikiliza shauri hilo leo kwa sababu amepewa nyaraka za mapingamizi saa saba kasoro (jana) na kama wakiamua hivyo, basi kesi ingeenda hadi saa tisa usiku.

Alidai ili haki itendeke, lazima wapewe muda wa kupitia na kujibu kwa sababu wapo mawakili sita, lakini waliofanikiwa kupitia ni watatu tu. Akapendekeza muda uongezwe na pia mapingamizi na maombi yasikilizwe kwa pamoja.

Katika shauri hilo, waleta maombi ni Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bubelwa Kaiza na Annanilea Nkya, ambao walifungua kesi ya kikatiba kwa kutaka Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ndiyo isimamie uchaguzi huo na si TAMISEMI.

# STARS YAPEWA NAFASI KUFUZU FAINALI AFCON

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) inaingia kambini kujiandaa na michezo miwili ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), zinatazofanyika mwakani nchini Morocco, makocha maarufu nchini, Mwinyi Zahera na Shadrack Nsajigwa, wameitabiria matokeo chanya Tanzania.

Wakizungumza jijini Dar es Salaam, makocha hao wamesema kwa sasa, Taifa Stars ni moja kati ya timu tishio Afrika, hivyo hawaoni sababu yoyote inayoweza kuifanya ishindwe kufuzu kucheza fainali hizo.

Zahera, ambaye kwa sasa anainoa Namungo, amesema alivyoiona AFCON iliyopita iliyochezwa Ivory Coast, na mechi kadhaa za kirafiki ilizocheza, Stars ina uwezo ule ule, hivyo ni timu tishio kwenye kundi hilo.

„Ninavyoiona timu ya taifa ya Tanzania inapanda uwezo siku hadi siku, nilivyoiona AFCON iliyopita na mechi kadhaa za kirafiki nilizoziona, nawapa asilimia nyingi za kufuzu fainali hizi.

Kuna timu mbili ambazo naona zitafuzu, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), ambayo ni lazima ifuzu, na timu nyingine ni Tanzania, ingawa Guinea nayo ina timu nzuri, lakini Stars kwa sasa ni moto wa kuotea mbali, „alisema kocha huyo wa zamani wa Yanga, Polisi Tanzania na Coastal Union ambaye ni Mkongomani.

Naye nahodha wa zamani wa Stars, Nsajigwa, alisema iwapo Stars itashinda mechi ya kwanza tu dhidi ya Ethiopia, basi itakuwa na nafasi kubwa ya kutinga fainali hizo.

„Tukiifunga Ethiopia tu basi utakuwa ni mwanzo mzuri sana, yaani wachezaji, viongozi na Watanzania wote watakuwa kitu kimoja, watakuwa vizuri kisaikolojia watakuwa wanaongea lugha moja kuhakikisha timu inafuzu. Kama tuliifunga Zambia kwao, ‚plani' iliyotumika tukiibadilisha kidogo tu tuna uwezo wa kushinda mechi hii hapa nyumbani," Nsajigwa alisema.

Aliongeza kikosi kilichoitwa kina uwezo wa kuifunga Ethiopia kwa sababu wachezaji wengi wanauzoefu na michuano ya kimataifa.

„Kwa kikosi kilichoitwa, na uwezo walionao Ethiopia kwa sasa, hatupishani sana, lakini sisi tuna wachezaji wapambanaji zaidi yao," aliongeza beki huyo wa zamani wa Yanga.

Kaimu Kocha Mkuu, Hemed Suleiman ‚Morocco' ameita wachezaji 23 kwa ajili ya kukabili Ethiopia Jumatano kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na mechi ya ugenini Guinea itakayochezwa Septemba 10, mwaka huu.

# Bodi, klabu zateta Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BODI ya Ligi Zanzibar imekutana na viongozi wa timu zinazotarajiwa kushiriki Ligi Kuu Zanzibar ili kujadili mambo mbalimbali kuelekea msimu mpya wa 2024/2025, imefahamika.

Msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar utaanza rasmi ifikapo Septemba 6, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa bodi hiyo, Issa Kassim Ali, alisema mambo makuu matatu yamejadiliwa ikiwamo viwanja vitakavyotumika, kanuni pamoja na maandalizi ya ratiba.

Ali alisema kikao hicho pia kilijadili na kukubaliana kwa baadhi ya mambo lakini wakiendelea kusubiri majibu kutoka serikalini kuhusiana na baadhi ya viwanja wanavyohitaji kutumia.

Alisema leo bodi hiyo inatarajia kukutana na viongozi wa klabu zitakazoshiriki Ligi ya Kanda ya Unguja na Pemba.

"Tunashukuru kikao chetu cha jana (juzi) kimeenda vizuri na kila kiongozi ameondoka akiwa ameridhika na yale ambayo tuliyakusudia kuyazungumzia," alisema ofisa huyo.

Aliongeza bodi hiyo imejipanga kuona mechi zote zinaandaliwa vyema ili kupata mabingwa ambao wamepatikana kwa haki.




Wachezaji wa Kagera Sugar FC wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya mabingwa watetezi, Yanga kutoka Dar es Salaam itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba mkoani Kagera. **PICHA: MTANDAO**

# Namungo yapania kuimaliza Fountain

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Mwinyi Zahera, amesema wachezaji wake wamejiandaa kurekebisha makosa katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Fountain Gate itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani Lindi.

Namungo ilikubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Tabora United katika mchezo wao wa kwanza uliochezwa ugenini kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zahera, alisema ameyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi iliyopita na anawataka wachezaji wake wasifikirie matokeo waliyopata wakiwa ugenini.

Zahera, kocha huyo wa zamani wa Yanga alisema licha ya kupoteza mechi hiyo, wachezaji wake walipambana na walijituma wakati wote wa mchezo huo.

"Kitu kikubwa ambacho alikiona katika mechi iliyopita ni hali ya kusikitika kwa wachezaji wake, kwa sababu hiyo alilazimika kuwapandisha morali ili kujiandaa kusaka pointi tatu muhimu kwenye mechi inayofuata, nimewaambia tuingia uwanjani tukiwa na nguvu mpya," Zahera alisema.

Hata hivyo aliongeza baada ya wapinzani wao kupata penalti, wachezaji wake walipoteza umakini na kutoa nafasi kwa wenyeji kumiliki mchezo.

Naye nahodha wa timu hiyo, Hamis Mgunya, alisema wachezaji wote wako vizuri kuelekea mechi ya leo na dhamira yao ni kupata ushindi.

Mgunya alisema anaamini mechi itakuwa ngumu lakini wao kama wenyeji wamejipanga kuhakikisha wanapata ushindi na ‚kufuta machozi' ya kupoteza mechi iliyopita.

"Mechi iliyopita tumeshaisahau, sasa hivi mipango yetu ni kuangalia mchezo ulioko mbele dhidi ya Fountain Gate, tumefanya maandalizi mazuri na sisi kama wachezaji tunaamini tutafanya vizuri, tumejiandaa vizuri zaidi na kwa sababu tutakuwa nyumbani, tunataka kuzibakisha pointi tatu kama tulivyopanga kabla ya msimu," nahodha huyo alisema.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo ni kati ya mabingwa watetezi, Yanga dhidi ya wenyeji Kagera Sugar.

## ZISIKUPITE

### CHELSEA YAMWINDA TONEY
CHELSEA inataka kumsajili mshambuliaji wa Brentford na Timu ya Taifa ya England, Ivan Toney, mwenye umri wa miaka 28. Hata hivyo The Blues hao hawatafikia mshahara unaopendekezwa na klabu ya Al-Ahli ya Saudi Arabia. (***Sky Sports***)

### WAARABU WAMTEGA TONEY
IVAN Toney anaweza kulipwa mshahara wa hadi pauni 400,000 kwa wiki akiamua kujiunga na klabu hiyo ya Al-Ahli ya Saudi Pro League. (***Mail***)

### CALVART-LEWIN AGEUKA LULU
KLABU za Newcastle United na Manchester United zinatazamia kumnunua mshambuliaji wa England, Dominic Calvert-Lewin, mwenye umri wa miaka 27, ambaye mkataba wake unamalizika Everton msimu ujao. (***Football Insider***)

### CHIESA ANUKIA LIVERPOOL
LIVERPOOL inawania kukamilisha usajili wa mshambuliaji wa Juventus na Timu ya Taifa ya Italia, Federico Chiesa, mwenye umri 26, kabla ya dirisha la uhamisho kufungwa hapo kesho. (***Athletic***)

### MANGALA AKARIBIA EVERTON
KIUNGO wa kati wa Lyon na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Orel Mangala, mwenye umri wa miaka 26, anatarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya na Everton kwa nia ya kujiunga na klabu hiyo kwa mkopo kabla ya tarehe ya mwisho ya uhamisho wa wachezaji. (***Sky Sports***)

### KHANNOUSS KUTUA LEICESTER
LEICESTER City inakaribia kufikia makubaliano katika ombi lao la pauni milioni 19.5 la kumnunua kiungo wa kati wa Genk na Timu ya Taifa ya Morocco, Bilal El Khannouss, mwenye umri wa miaka 20. (***Daily Telegraph***)

### BROBBEY ATAJWA FOREST
KLABU ya Nottingham Forest inamnyatia mshambuliaji wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Brian Brobbey, mwenye umri wa miaka 22, na huenda wakamsajili kabla ya dirisha la uhamisho kufungwa. (***Mirror***)

### DURAN KUMRITHI OSIMHEN
CHELSEA itamsajili mshambuliaji wa Aston Villa na Timu ya Taifa ya Colombia, Jhon Duran, mwenye umri wa miaka 20, endapo watashindwa kumsajili mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen (25). (***Givemesport***)

### ROMA YAMTAJA ABRAHAM
AS Roma wako tayari kumuuza mshambuliaji wa England, Tammy Abraham, mwenye umri wa miaka 26, huku West Ham wakionyesha nia ya kumtaka nyota huyo. (***Football Insider***)

### BAYERN YAMFUATA SANCHO
BAYERN Munich na Borussia Dortmund zinafuatilia hali ya winga wa England, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 24 katika klabu yake ya Manchester United. (***Sportsport***)

### CITY, NUNES NJIA PANDA
MANCHESTER City bado haijafanya uamuzi kuhusu mustakabali wa kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ureno, Matheus Nunes, mwenye umri wa miaka 25, lakini wanajua Atletico Madrid wana nia ya kumnunua. (***ESPN***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MAMADASHVILI RASMI ASAJILIWA LIVERPOOL

**LIVERPOOL,** England

**Lakini ataanza kuitumikia timu yake hiyo mpya mwakani...**

LIVERPOOL imethibitisha rasmi imefikia makubaliano ya kumsajili mlinda mlango wa Valencia, Giorgi Mamadashvili, ambaye atajiunga na klabu hiyo msimu ujao wa joto.

**Wekundu hao bado hawa jaimarisha kikosi cha Arne Slot msimu huu wa joto la kini badala yake wamepa nia kukamilisha dili la Mamadashvili, ambaye anatajwa kuchukua nafasi ya muda mrefu ya mchezaji wa kimataifa wa Brazil, Alisson.**

Baada ya mazungumzo ya wiki kadhaa, Liverpool sasa wamethibitisha wamefikia makubaliano ya kumsajili Mamadashvili, ambaye atasalia na Valencia kwa muda uliosalia wa msimu huu kabla ya kuhamia Anfield hapo mwakani.

Taarifa kutoka kwa klabu zote mbili hazihitaji mkopo wowote, badala yake zinasisitiza Mamadashvili atajiunga na Liverpool kabisa mwaka ujao.

Hata hivyo, The Athletic limeripoti wanaelezea mpango huo kama mkopo.

Alisson tayari ameungwa mkono na umma kuhusu uhamisho huo, akikiri anaelewa nia ya Liverpool ya kupanga maisha ya baadaye.

Mamardashvili, ambaye atatimiza umri wa miaka 24 Septemba, mwaka huu tayari ameshaichezea Valencia zaidi ya mechi 100 na anasifiwa sana kama mmoja wa makipa bora chipukizi duniani.

Hisa zake ziliimarishwa zaidi msimu huu wa joto na maonyesho bora ya Georgia kwenye Euro 2024.

Wakati huo huo, Caoimhin Kelleher anasalia kuwa mbadala wa Liverpool kwa sasa, ingawa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amekiri wazi yuko tayari kuondoka Anfield kutafuta nafasi ya kuanza baada ya miaka mingi nyuma ya Alisson katika orodha ya wachezaji wanaocheza soka la kulipwa.

# WAARABU WAKANA OFA NONO YA VINICIUS JR




**RIYADH,** Saudi Arabia

KLABU ya Ligi Kuu ya Saudi Arabia, Saudi Pro League, Al Ahli haijawahi kutoa ofa nzito kumsajili supastaa wa Real Madrid, Vinicius Junior, licha ya madai ya kutaka kuweka rekodi ya dunia, kwa mujibu wa 90.

Vini Jr., mshindani mkuu wa Ballon d'Or 2024, amekuwa akihusishwa mara kwa mara na Saudi Arabia msimu huu wa joto.

Kutoka Hispania wiki hii, kumekuwa na madai ya ofa ya euro milioni 500 kutoka kwa Al Ahli na mkataba wenye thamani ya euro bilioni moja kwa kipindi cha miaka mitano, pamoja na uwezekano wa bonasi.

Vyanzo vya habari nchini Saudi Arabia vimekanusha kuwapo kwa pendekezo lolote kama hilo. Ni kawaida katika hali hizi kwa waamuzi kufikia na pengine hata kuwasiliana na ofa ya msingi ili kupima maslahi yanayoweza kutokea.

Lakini hakuna uthibitisho majaribio ya maana yamefanywa katika kesi hii na haijawahi kuwa hisia winga huyo wa Real Madrid angewaniwa.

Viongozi wa soka Saudi Arabia hawana siri katika kutaka wachezaji bora zaidi kwenye ligi yao, lakini kuna ufahamu Vinicius Junior hatafanya mabadiliko hayo hivi sasa.

Wachezaji wa hadhi ya juu wanaolengwa katika kipindi kilichosalia cha dirisha la usajili la majira ya kiangazi ni mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen, ambaye wakala wake amedokeza hadharani kusita kuondoka Ulaya katika kipindi hiki cha maisha yake ya soka, na winga wa Bayern Munich, Kingsley Coman.

Mchezaji wa Brentford, Ivan Toney ni jina lingine ambalo wafanyabiashara wapo kwenye mazungumzo, wakati Joao Cancelo amesaini Al Hilal kwa mkataba wenye thamani ya euro milioni 25.

Saudi Arabia inatazamiwa kuwa mwenyeji wa michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2034, ikiwa haijapingwa wakati wa ofa yao, na wizara ya utalii imefikia kambi ya Vinicius kuhusu uwezekano wa kumnadi ili kukuza mashindano hayo kwa niaba ya nchi.

Kwa sasa, hakuna ofa na Vinicius Junior hatahamia Saudi Arabia.

# Cancelo atimkia Saudi Arabia

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City imethibitisha kuachana na beki wake wa pembeni, Joao Cancelo, ambaye amejiunga na klabu ya Al Hilal ya Saudi Arabia kwa uhamisho wa kudumu.

Cancelo hajaichezea Manchester City mechi ya ushindani tangu alipokosa kikosi cha kwanza ghafla katikati ya msimu wa 2022/23 na kujiunga na Bayern Munich kwa mkopo Januari hiyo.



Mreno huyo alikaa msimu uliopita akiwa na Barcelona lakini alirejea Manchester City muda huo ulipoisha.

Pep Guardiola hakumtenga Cancelo, ambaye alikuwa haridhishwi na jukumu lake huku ushindani ukiongezeka kutoka kwa Nathan Ake na Rico Lewis, kusalia na kujumuishwa tena msimu huu, lakini kuhamia Al Hilal sasa kumekamilika.

"Ningependa kuwatakia kila mmoja katika City mafanikio katika siku zijazo," alisema Cancelo baada ya kuhitimisha kile kinachodaiwa usajili wa pauni milioni 21.

"Nilikuwa na nyakati nyingi za kipekee wakati wangu pale kwenye klabu kubwa.

"Ningependa kuwashukuru wachezaji wenzangu, makocha, wafanyakazi wote wa City na mashabiki kwa kila kitu katika muda wangu hapa."

Cancelo anaripotiwa kulipwa mshahara wa jumla wa euro milioni 15 kwa msimu kwa miaka mitatu ijayo.

City hapo awali ilimsajili Cancelo kutoka Juventus kwa mkataba uliomjumuisha Danilo kuelekea upande tofauti, wenye thamani ya hadi pauni milioni 60 msimu wa joto wa mwaka 2019.

Akiwa Al Hilal, ataungana na mchezaji mwenzake wa kimataifa wa Ureno, Ruben Neves, na nyota wengine wanaozungumza Kireno akiwamo Neymar, Malcom na Renan Lodi, wanaocheza chini ya Kocha, Jorge Jesus, ambaye ni Mreno.

Ili kumpa nafasi Cancelo, Saud Abdulhamid, amefanya uhamisho wa kihistoria kwenda Roma.

Inaelekea kumfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ambaye alikuwa kwenye Kombe la Dunia la mwaka 2022, kuwa mchezaji wa kwanza kabisa kutoka Saudi Arabia kuonekana katika mojawapo ya ligi tano bora za Ulaya - EPL, La Liga, Serie A, Bundesliga au Ligue 1.

Kihistoria, wachezaji wachache sana kutoka taifa hilo lenye utajiri mkubwa wa mafuta wamewahi kuhamia nje ya nchi.

Al Hilal walipanda Ligi Kuu ya Saudia msimu uliopita na tayari wako kileleni tena baada ya kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Al Okhdood katika mechi ya ufunguzi iliyochezwa Jumamosi iliyopita.

## Olmo asherehekea bao la ndoto Barca

**BARCELONA,** Hispania

DANI Olmo alisherehekea „ndoto ya kwanza" aliporejea Barcelona alipofunga bao la ushindi katika mechi iliyomalizika kwa magoli 2-1 dhidi ya Rayo Vallecano katika Ligi Kuu ya Hispania maarufu LaLiga.

Olmo mwenye umri wa miaka 26, alikosa michezo miwili ya kwanza ya Barca msimu huu huku timu hiyo ya Katalunya haikufanikiwa kumsajili kwa sababu walibakia kuvuka kiwango cha matumizi kilichowekwa kwenye ligi, lakini usajili wake hatimaye ulishughulikiwa wiki hii na akaleta matokeo juzi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania aliingia akitokea benchi wakati wa mapumziko na akafunga bao muhimu dakika ya 82 huku Barca wakishinda mara tatu katika mechi tatu msimu huu baada ya Pedri kusawazisha goli la Unai López dakika ya tisa.

"Nina furaha sana na mchezo wa ushindi," alisema Olmo akiiambia ESPN. „Ilikuwa ndoto yangu ya kwanza."

Olmo alilazimika kusubiri kucheza mechi yake ya kwanza ya ushindani baada ya kusaini mkataba wa Euro milioni 55 kutoka RB Leipzig mapema msimu huu wa joto kufuatia uchezaji wake wa kuvutia akiwa na Hispania wakati La Roja ikitwaa ubingwa wa Ulaya.

Hata hivyo, fowadi huyo mahiri, ambaye alipitia akademi ya Barca kabla ya kwenda Dinamo Zagreb akiwa na umri wa miaka 16, alisema kila mara anaamini klabu hiyo itasuluhisha matatizo ya kifedha yanayozuia usajili wake.

"Ilikuwa ndoto, bila shaka, kurudi," aliongeza Olmo. „Sikuwa na shaka wakati Barcelona ilipobisha mlango wangu. Kwa hiyo nina furaha sana kuwa hapa.

"Nilikuwa na imani klabu itasuluhisha usajili. Nilikuwa tayari, nikijiandaa kimwili wakati nilipata nafasi ya kuanza kucheza. Leo ningeweza kufanya hivyo, kwa kweli, nina furaha sana jinsi ilivyokuwa, jinsi ilivyokuwa kumaliza na jinsi ilivyokuwa muhimu sana kwa timu."

Kocha wa Barca, Hansi Flick, naye alifurahishwa na uchezaji wa Olmo baada ya kumleta pamoja na Ferran Torres wakati wa mapumziko na timu yake ikiwa nyuma kwa bao 1-0.

"Alikuwa akisubiri kwa muda mrefu kufunga bao kwa Barca," alisema Flick katika mkutano na waandishi wa habari.

"Alipoingia uliona tulikuwa na udhibiti zaidi na mpira. Ilikuwa nzuri sana.

"Kwake yeye analeta hivyo, kumiliki mpira ni salama na pia mbele ya goli anajua kufunga, kwa mchezaji wa kiungo sio kawaida, lakini yuko vizuri sana katika hili."

## Ateba kuiongoza Simba...

INATOKA UKURASA 24

atamchezesha Valentino Mashaka, nyota ambaye ameanza kumpa mwanga mzuri katika kikosi chake.

"Steven Mukwala yeye amekwenda katika kikosi chake cha timu ya taifa ya Uganda, kwa mastraika nimebakia na Mashaka, atasaidiana na Ateba, ni straika mzuri sana na mmeona kila akitokea benchi anafunga katika michezo yote miwili ambayo amecheza," alisema kocha huyo.

Mashaka ambaye kabla ya mechi za Ligi Kuu jana alikuwa anaongoza kwa kupachika mabao, akiwa na mabao mawili, akiyafunga katika mechi mbili tofauti, dhidi ya Tabora United, Simba ikishinda mabao 3-0 na dhidi ya Fountain Gate, ikishinda mabao 4-0 na zote akitokea kwenye benchi.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amethibitisha Ateba kwamba ana kila kitu ambacho kinamruhusu kucheza, hivyo kuwataka mashabiki wa soka kujitokeza kwa wingi kumuona kwa mara ya kwanza straika huyo akiwa na uzi mwekundu.

Ahmed alisema wameamua kuandaa mchezo huo wa kirafiki ili kuwajenga zaidi wachezaji wao kwa sababu wanahitaji kufanya vizuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa wanayoshiriki.

Wakati Simba ikijiandaa kucheza dhidi ya Al Ahly Tripoli huku Al Hilal nayo inajiandaa kucheza mchezo wa raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya San Pedro ya Ivory Coast, baada ya kuing'oa, Al Ahly Benghazi ya Libya, kwa jumla ya mabao 2-1, ikishinda bao 1-0 ugenini na kutoka sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Juba, nchini Sudan Kusini.



# BAO WAOMBA KUPELEKWA KUSHINDANA KAZAKHSTAN

**Na Faustine Feliciane**

SHIRIKISHO la Bao Tanzania (SHIMBATA), limeiomba serikali kuwasaidia kushiriki mashindano ya mchezo huo yaliyopangwa kufanyika kuanzia Septemba 8 hadi 14, mwaka huu nchini Kazakhstan.

Akizungumza katika ofisi za gazeti hili zilizopo Mikocheni, Dar es Salaam jana, Rais wa SHIMBATA, Mande Likwepa, alisema wamepokea mwaliko wa kushiriki mashindano hayo yatakayofanyika kwenye Jiji la Astana lakini wanashindwa kuthibitisha mapema kwa sababu ya kukosa fedha.

Likwepa alisema ili kupeleka timu katika mashindano hayo wanahitaji kupata Sh. milioni 15 na tayari wameshapeleka maombi katika Baraza la Michezo la Taifa (BMT).

"Walitupa mwaliko wa watu 15 na walikuwa tayari kugharamikia tiketi na malazi ya watu sita, na sisi tuwalipie waliobakia, kwa bahati mbaya tumewasilisha barua mwaliko na kuomba kusaidiwa kwa BMT, wenzetu walichelewa kutujibu na sisi kushindwa kuthibitisha mapema ushiriki wetu," alisema Likwepa.

Aliongeza baada ya kushindwa kupeleka idadi hiyo ya watu, wanaiomba serikali kusaidia kupeleka wachezaji wanne na kiongozi mmoja ili kutoipoteza nafasi hiyo muhimu ya kuitangaza nchi.

"Zimebaki siku chache sana kabla ya mashindano haya kuanza, tunaomba serikali itusaidie kupeleka angalau wachezaji wanne na kiongozi mmoja ili nasi tukashiriki na kuweka historia," Likwepa alisema.

Rais wa huyo alisema kwa kiasi kikubwa wamefanikiwa kuutangaza mchezo huo na kutambulika kimataifa na wanaamini wameendeleza juhudi za Baba wa Taifa, Julius Nyerere ambaye alikuwa na mapenzi makubwa na mchezo huo.

"Hayati Baba wa Taifa alikuwa na mapenzi na mchezo huu na hata wakati anatoka madarakani alimkabidhi Rais Ali Hassan Mwinyi aendeleze usipotee, na sisi kumuunga mkono tukaanzisha shirikisho la mchezo huu ambalo linaendelea kuutangaza," alisema Likwepa.



Kikundi cha Ngoma ya Asili cha Twiyende kikitumbuiza katika tamasha lililoandaliwa na Shirika la Jinsia la TGNP lililofanyika katika Mji wa Kondoa jijini, Dodoma jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Baiskeli kushindana Oktoba Tabora

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Baiskeli Tanzania (CHABATA), kimeandaa mashindano ya mchezo huo yatafayofanyika kuanzia Oktoba 10 hadi 14, mwaka huu mkoani Tabora.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa CHABATA, Godfrey Mhagama, alisema washiriki wa shindano hilo watatoka katika nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Mhagama alisema maandalizi ya shindano hilo yanaendelea vizuri na wanaamini yatatoa fursa kwa washiriki kuonesha vipaji vyao huku mwisho wa washiriki kuthibitisha ni Oktoba Mosi, mwaka huu.

„Kwa sasa tunaendelea kufanya maandalizi kwa ajili ya shindano hilo lenye lengo la kumwenzi Rais wa kwanza wa Tanzania Marehemu Mwalimu Julius Nyerere," alisema Mhagama.

Alitaja nchi zilizothibitisha kushiriki ni pamoja na Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Sudan Kusini, Malawi na Afrika Kusini.

Aliongeza CHABATA inaendelea kufanya mazungumzo na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ili kuisaidia Timu ya Tanzania kupata maandalizi mazuri huku akiyaomba makampuni na taasisi mbalimbali kuwaunga mkono katika kufanikisha shindano hilo.

# Gamondi atamba kuanza ligi kibabe

INATOKA UK. 24

"Mchezo utakuwa mgumu kwa sababu kwanza tunacheza ugenini, lakini wenzetu walifungwa mechi iliyopita kwa hiyo wanataka kushinda katika mchezo huu wa pili, sisi pia tunataka kushinda kwa sababu ni mchezo wa kwanza kwetu kwenye ligi haitapendeza kama hatutapata matokeo mazuri zaidi ya hayo," alisema Job.

Naye Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Paul Nkata, aliliambia gazeti hili wanakwenda kucheza na timu kubwa iliyofanya vyema katika mechi za kimataifa, hivyo wataingia kwa tahadhari kubwa.

Nkata alisema amewaandaa wachezaji wake kucheza kwa nidhamu na kutowapa nafasi nyota wa Yanga kumiliki mchezo kwa sababu itawasababishia ,hatari; upande wao.

"Tutacheza tukiwa nyumbani, lakini na timu kubwa ambayo imefanya vyema katika michezo ya kimataifa, lakini tumejipanga, yale makosa yaliyoonekana katika mchezo wetu uliopita tukapoteza tumejaribu kuyarekebisha, nadhani tutakuwa na mchezo mzuri," alisema Nkata, kocha huyo raia huyo wa Uganda.

Kagera Sugar itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0 na Singida Black Stars, mechi ikichezwa hapo hapo Bukoba wakati Yanga wao walipata ushindi mnono wa mabao 6-0 dhidi ya Vital'O katika mchezo wa mkondo wa pili wa michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya awali kuwachapa magoli 4-0.

Mechi zingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya KMC dhidi ya Coastal Union wakati kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa, wenyeji Namungo itawaalika Fountain Gate.

Simba yenye pointi sita ndio inaongoza ligi hiyo baada ya mechi yake ya kwanza kuwafunga Tabora United mabao 3-0 na iliposhuka tena kwenye Uwanja wa KMC iliwachapa Fountain Gate magoli 4-0.



# Michezo

Nipashe

Alhamisi Agosti 29, 2024




Cancelo atimkia Saudi Arabia UKURASA 22



Winga wa Azam FC, Gibril Sillah (kushoto), akijiandaa kumtoka beki wa JKT Tanzania, Maka Edward (kulia), katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Isamhuyo, Dar es Salaam jana. **PICHA: MTANDAO**

## Ateba kuiongoza Simba Jumamosi

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA mpya Mkamerooon Leonel Ateba anatarajia kuongoza safu ya ushambuliaji ya Simba katika mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Al Hilal kutoka Sudan itakayochezwa kesho kutwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam imefahamika.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema anatarajiwa kumtumia straika huyo aliyesajiliwa kutoka USM Alger ya Algeria ambaye hakumpanga katika mchezo uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Fountain Gate kutokana na taratibu za vibali kutokamilika.

Fadlu alisema kwa sasa taratibu zote za kumtumia mchezaji huyo zimekamilika hivyo ataongoza mashambulizi katika mchezo huo ambao ni maalum kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya raundi ya kwanza ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahly Tripoli ya Libya.

„Sikumtumia sio kwa sababu za kiufundi, ila alikuwa na matatizo ya vibali, kwa sasa kila kitu kipo tayari, nitamtumia katika mchezo huo ili kumweka sawa, azoeane na wenzake kuelekea katika mechi yetu ya Kombe la Shirikisho,“ alisema kocha huyo.

Ateba ni mchezaji wa mwisho kusajiliwa na Wekundu wa Msimbazi, akiwa ni mbadala wa Freddy Michael, ambaye inasemekana kocha huyo hakuridhika naye, hivyo kuwataka mabosi wa klabu hiyo kumtafutia straika mwingine kabla ya kufungwa kwa dirisha kubwa la usajili.

Hata hivyo, Fadlu alisema pamoja na kutarajia kumchezesha straika huyo, pia

INAENDELEA UK. 23

# GAMONDI ATAMBA KUANZA LIGI KIBABE

●●● Kocha huyo asema anaifahamu vyema Kagera na amewaandalia......

**Adam Fungamwango na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kutoa ‚dozi nzito‘ katika mashindano ya kimataifa, Yanga inatarajia kuanza rasmi kutetea Ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kuwakabili wenyeji Kagera Sugar katika mechi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba mkoani Kagera.

Yanga iliyoichapa Vital'O ya Burundi jumla ya mabao 10-0, Azam FC na Coastal Union zimechelewa kuanza Ligi Kuu Tanzania Bara kutokana na kukabiliwa na mechi za awali za mashindano ya kimataifa yanayosimamiwa na kuandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema wanawafahamu vyema wapinzani wao Kagera Sugar kuwa ni timu nzuri na ngumu.

Gamondi alisema mechi hiyo haitakuwa nyepesi kwa sababu wanaenda kukutana na moja ya timu ngumu katika Ligi Kuu Tanzania Bara na yenye wachezaji wazoefu.

Kocha huyo alisema anafahamu na anakumbuka vizuri Kagera Sugar iliyowasumbua katika mechi ya mzunguko wa kwanza msimu uliopita ambayo ilichezwa Mei 12, mwaka jana, ambapo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1, tena ikichezwa kwenye uwanja huohuo.

"Kagera Sugar naifahamu, ni timu ngumu, tunaiheshimu, tumejiandaa kwa ajili ya kupambana na timu ya aina hiyo, ikizingatia tunacheza ugenini na timu hii kwenye uwanja ambao ni mgumu, hatujauzoea na hata ubora wake si mzuri sana ingawa ni wa nyasi bandia, lakini sisi tuna uzoefu,“ alisema Gamondi.

Aliongeza anahitaji kuanza msimu mpya kwa ushindi kwa sababu anataka kufikia malengo yake kama timu na wakati wote atacheza kwa kuwaheshimu wapinzani wao.

Nahodha Msaidizi wa Yanga, Dickson Job, amekiri wanatarajia mchezo huo utakuwa mgumu kutokana na aina ya timu zinazokutana.

Job alisema kila mchezaji yuko tayari kwa mechi hiyo na wanaamini wanaenda kuendeleza furaha kwa wanachama na mashabiki wao.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >